# *KUINGIA KATIKA ROHO*

Ajabu, nilikuwa nimesimama hapa nikizungumza juu ya Ndugu David, ninaamini, jana usiku, naye huyu hapa anatokea jukwaani usiku wa leo. Vema, hilo ni sawa kabisa.

2 Ndugu David, tuna furaha kuwa pamoja nawe hapa Chicago. Na ni vizuri kuwa nanyi ndugu nyuma yangu hapa, usiku wa leo, kujua msaada wenu katika maombi sasa ni wangu, ninapoutangaza Ujumbe wa Bwana; iweni katika maombi kwa ajili yangu.

3 Ni vizuri kuwa nje tena usiku wa leo hapa ukumbini, tumeketi vizuri sana huku nje, pamoja na watu. Na chini ya matarajio ya kuona kazi, na, ya—ya Roho Mtakatifu, kuja miongoni mwetu tena, usiku wa leo.

4 Bila shaka tumefurahia kila saa ya ibada hii, tukiwa hapa. Kuna . . . Tangu Jumapili iliyopita jioni, ama Jumapili iliyopita alasiri, hasa, tulikuwa na wakati mzuri sana, wa ajabu, naye Roho Mtakatifu ametenda mambo makuu miongoni mwetu. Tumemwona akiwaponya wagonjwa, na kufanya miujiza, na kuwaokoa watu, na kuwajaza na Roho Mtakatifu, na mambo makuu tu. Tungeweza kumwomba nini zaidi ya hayo na yale tumemwona akifanya?

5 Na nina furaha sana kujua ya kwamba tunaishi katika siku ya mwisho, na kama wahudumu wa Injili, tuna majaliwa ya kuwazungumzia, naamini, Wateule wa Mungu katika siku za mwisho. Na ni majaliwa ya jinsi gani kwetu sisi wahudumu kuwa na majaliwa haya ya kuketi hapa duniani leo, na kuuzungumzia wakati wa mwisho wa kanisa, Kanisa la mwisho!

6 Ninaamini kwamba, kweli, kwa moyo wangu wote kwamba sasa tunauzungumzia wakati wa mwisho wa kanisa, ambao hatimaye utaishia katika Kanisa la Laodikia na ndipo tutaninii . . . Yesu atakuja na yote yatakwisha. Nami nitafurahi hilo litakapotukia.

7 Ninajisikia kama Yohana wa kale, "Hata hivyo, njoo, Bwana Yesu." Kasema, "Hata hivyo." Karibu nimeona ya kutosha. Nilikuwa nikizunguka, na inaonekana kama badala ya kuwa bora, mbona, ulimwengu unazidi kuwa mwovu wakati wote. Kwa hiyo na—nafikiri kama Yohana alivyosema, "Hata hivyo, njoo, Bwana Yesu," ndipo yote yatakwisha.

8 Nami, naona wangali wana kitabu hiki kidogo, kilicho hapa, cha ono lililochapishwa. Na kila ninapowazia jambo hilo, moyo wangu unawaka moto nipate kuingia zaidi mkutanoni, kufanya jambo fulani mara moja, kwa sababu ni, haitachukua muda mrefu mpaka, labda, hatutakuwa na wakati wa kufanya lolote.

Kwa hiyo tunataka kufanya hivyo sasa, wakati tunapoweza kulifanya. Basi Bwana na aongeze baraka Zake, usiku wa leo, tena.

9 Sasa, kesho asubuhi ni kiamshakinywa cha Wafanyabiashara, naamini, papa hapa uwanjani. Ninaamini wao. . .Tayari imetangazwa, ya kwamba kutakuwa na kiamshakinywa cha Wafanyabiashara kesho. Nami nafikiri umma umealikwa kwenye hiki. Bora tu uje, mbona, tutafurahi sana.

10 Nayo ni zamu yangu asubuhi, kama likimpendeza Mungu, ku—kuzungumza, angalau mmoja wa wasemaji, kwenye kiamshakinywa. Nami ninatumaini ya kwamba Bwana atakutana na sisi sote, na kama hujawahi kuhudhuria moja ya viamshakinywa hivi, baadhi yenu ninyi wafanyabiashara hapa, wa mjini, hakika ingekufaa kuja na kusikia yale Mungu amewafanyia wafanyabiashara wengine.

11 Sasa, huenda ukawa mtu aliyefanikiwa, kuhusu ninii. . . kuhusu biashara yako, bali hatujaribu kukuletea kitu fulani kukufanya bora zaidi, ama—ama, kuifanya biashara yako kuwa bora zaidi, tunajaribu kukuletea Kitu fulani ambacho kitakufanya *wewe* bora zaidi, Hicho ni—Hicho ni Kristo, unaona, Kristo.

12 Kama nilivyosema hivi majuzi usiku, Kanisa lilipoteza mpango wake kwa muda mrefu wakati lilipojaribu kujilinganisha na ulimwengu, pamoja na elimu, na kuchezacheza, na pamoja na burudani, na kadhalika. Ha—ha—hatutalinganishwa nao kamwe, watoto wa usiku ni werevu kuliko watoto wa mchana, wana hekima zaidi, Yesu alisema hivyo.

13 Wala hatungeweza kamwe kuwapa burudani, na—na hata hivyo, Injili si mng'ao, ni mwako, mnaona, ni mwako, laini na mtamu. Nasi. . .Kuna Kitu kimoja tu tulicho nacho ambacho ulimwengu hauna, wala hauwezi kuwa nacho isipokuwa wawe mmoja wetu, tunaye Yesu, ndivyo hivyo, tunaye Yesu.

14 Sisi si werevu kama walivyo, hatujaendelea sana katika sayansi, hatujui lolote kuihusu hiyo. Wala hatujaribu kushindana nao katika. . .kuwa na e—elimu bora, ama shule bora zaidi, ama kadhalika, na kusema, "Kanisa letu lina shule *hii*," na kadhalika. Hiyo ni sawa katika njia hiyo, bali tunaye Yesu, huyo Ndiye tunayejaribu kumleta kwa walimwengu, ni Yesu Kristo. Naye ni Mwana wa Mungu, Naye ni Mwokozi wetu, nasi tunamjua katika nguvu za kufufuka Kwake, na hicho ndicho kitu halisi.

15 Sasa, baadhi yetu ni. . .Jamani, kwangu mimi, sijui, labda, sikijui Kitabu Chake vizuri sana, lakini ni—ninamjua Yeye vizuri sana. Na hiyo ni. . .Naye. . .Ni, yote ninayopaswa kujua ni kumjua Yeye. Kujua Kitabu Chake hakukupi Uzima wa Milele,

bali kumjua Yeye ni Uzima, kumjua Yeye, huyo Mtu wa hicho Kitabu, ni Uzima.

16 Sasa, kesho usiku tena, basi tunatarajia, Bwana akipenda, kuwa na ibada nyingine ya uponyaji. Halafu kesho, ama, Jumapili alasiri inafunga mkutano huu, kisha niondoke, basi, kwenda kaskazini mwa British Columbia, na Dawson Creek, na Grande Prairie, na Fort Saint John, na kupitia sehemu hiyo ya nchi huko juu, kwa ninii, labda, wakati uliosalia wa kiangazi. Kwa hiyo iweni mkituombea sasa. Nasi tunatumaini kuwaona kwenye kiamshakinywa asubuhi, na kuendelea na mkutano wote.

17 Sasa, na msisahau sasa, ninyi wageni, ndugu hawa wote hapa usiku wa leo, sababu ya wao kuketi hapa, ni kwa sababu wao ni wahudumu wa Injili ii hii. Basi tafuta mahali makanisa yao yalipo na muwajazie hayo Jumapili asubuhi, sasa, kwa mkutano mkubwa. Tunatumaini tu utaacha uamsho mzuri, mzuri sana, ukienea tu kote mjini, na, mpaka Yesu atakapokuja.

18 Sasa, maskini Joseph hapa, Boze, daima ameniambia jambo hilo, miaka mingi iliyopita, huko nje kwenye Barabara ya Lake Shore, tulipoketi siku moja, naye akasema, katika Kiingereza chake kibovu, "*Tugu* Branham, daima tumekuwa na hisia moyoni mwangu kwamba nilitaka kuona Chicago ikitikiswa, nataka kuona Chicago ikitikiswa." Kasema, "Miaka mingi iliyopita, nilitoka hapa New York nipate kuona Chicago ikitikiswa."

19 Hivi majuzi asubuhi, kabla tu ya mahojiano yangu, nilikula kiamshakinywa pamoja na Joseph, na sikuzote nimempenda sana, na kwa hiyo basi, nikasema, "Ndugu Joseph, sha—shauku yako kuu imetimizwa, ila tu siamini unajua, unaelewa hilo." Mnaona? "Unapozungumza kuhusu, 'kuutikisa mji; kulitikisa taifa,' hilo halimaanishi hiki hapa chakula cha atomiki kinachozungukazunguka hapa, hilo linamaanisha Kanisa, Kanisa ndilo linalotikiswa, ninii tu, si hilo kundi la kikanisa, bali Mwi—Mwili wa Kristo, huo ndio unaotikisika na kurudi m—mstarini tena."

20 Nao, hilo kundi la Chicago linaninii, linajua hiyo ni kweli, kwamba wamekuwa na mtikiso halisi katika miaka michache iliyopita, katika miaka hii sita au saba iliyopita. Jinsi ambavyo watu mashuhuri wa Mungu wamekuja kwenye mji huu na kuwahubiria Wateule, na ishara na maajabu na miujiza imetendeka, mpaka kwamba hamna udhuru, kabisa, hamna udhuru, ni, "Tubuni ama mwangamie," hivyo tu.

21 Sasa, ninyi mnaoweka hesabu ya, ama, mnaoandika mafungu, kama tungeyaita, nina Maandiko machache na—na muhtasari ulioandikwa hapa usiku wa leo, juu ya somo dogo ambalo ninapaswa kulimalizia ndani, ifikapo saa tano,

baadaye kidogo. Na kwa hiyo. . .Mimi, jana usiku nilininii. . . [Kusanyiko linashangilia—Mh.] Asanteni, hilo ni zuri kwenu.

22 Kila usiku, Billy alisema, "Ninataka kuona utakapoenda Chicago, kama unaweza kumalizia usiku mmoja, mnamo, saa tatu na nusu, nataka kuona kama mnaweza kufanya hivyo."

"Loo," nikasema, "hiyo itakuwa rahisi, nitahubiri tu dakika ishirini usiku wowote."

Kila usiku, wanapoondoka, alisema, "Uliikosa kiasi gani usiku wa leo?"

23 Nikasema, "Zaidi ya saa mbili hasa, kitu kama hicho." Lakini si—sijui sana, bali ninapenda tu kuendelea kusimulia yale nijuayo, kwa hiyo, mpaka yanapozama ndani.

24 Maskini mhudumu mmoja wakati mmoja, alienda kanisani. Ninajua hapa si mahali pa kufanyia mzaha, simaanishi hili katika mizaha, bali ni kwamba tu nipate kubadilisha njia ya kuwazia kwa muda mfupi tu. Alienda kwenye kanisa fulani, ndipo usiku wa kwanza aliohubiri ulikuwa ni juu ya "Tubuni." Usiku wa pili aliohubiri, ulikuwa juu ya "Tubuni." Usiku wa tatu, wa nne, wa tano, wa sita, alihubiri juu ya "Tubuni."

25 Vema, hilo lilikuwa sawa. Kwa hiyo wazee wa kanisa wakamwita na kusema, "Daktari," kasema, "tunathamini ujumbe wako juu ya kutubu, lakini kwa siku sita usiku mfululizo, umehubiri ujumbe ule ule, juu ya toba."

Akasema, "Loo, vema, hilo ni sawa."

Kasema, "Kwani huna ujumbe mwingine?"

26 Akasema, "Loo, naam, lakini hebu wote watubu kwanza, ndipo nitahubiri juu ya jambo lingine, mnaona." Kwa hiyo, jambo ndilo hilo. Baada ya wote kutubu, vema basi atahubiri juu ya jambo lingine. Kwa hiyo hiyo ni falsafa nzuri sana, mnaona. Tubuni mpaka sisi sote tumetubu, hilo lingekuwa jambo zuri, nina hakika tungekuwa hapa kwa muda mrefu.

27 Katika Wafalme wa Pili, mlango wa 3, nami ninataka kusoma kifungu cha 15:

> *Ila sasa nileteeni mpiga kinanda. Ikawa, mpiga kinanda alipokipiga, mkono wa* B*WANA* *ukamjia juu yake.*

28 Na kama ningetaka kuvuta kutoka hapo somo, nipate kutoa muktadha, huenda nikachukua somo hili hapa: *Kuingia Katika Roho*.

29 Kulikuwa na badiliko kubwa lililotukia kote Palestina siku hizi, jambo moja kuu lilikuwa limetukia, yule nabii mkuu mashuhuri, alikuwa amehamishwa, akatwaliwa juu Utukufuni. Na ilikuwa ni hasara kubwa kwa Kanisa, wakati mtu mashuhuri kama huyo anapoondolewa.

30 Lakini ni faraja jinsi gani hilo lilipaswa kuliletea taifa hilo, ambalo lilikuwa ndilo Kanisa wakati huo, kujua ya kwamba mtu huyu, akiisha kutumwa kwao kumwakilisha Mungu, alikuwa ameenda Nyumbani bila hata kufa, ambaye alikuwa amenyakuliwa na kutwaliwa juu. Eliya, alikuwa mfano mzuri sana, wa siku hizi.

31 Wakati, huenda ikawa ni mbali kidogo na njia inayokubalika na mtu aijuaye Biblia vizuri kuliko mimi, lakini kwa namna fulani ninaamini ya kwamba kutakuwako na Ujumbe katika siku za mwisho, kitu kama Eliya, na kwamba Kanisa linalofanana na Eliya, litakuwa ninii, halitakufa bali litahamishwa, kutwaliwa juu, Moto utalipeleka Utukufuni, Moto wa Kipentekoste utalinyakua.

32 Hata hivyo, Mungu daima hufanya nji—njia kwa ajili ya Kanisa Lake, wakati Yeye amemalizana na mtu mmoja, anaye mwingine anayengojea. Naye Mungu humchukua mtu Wake, bali kamwe si roho yake, Yeye daima ana mtu mwingine anayeweza kuwekea roho yake juu yake.

33 Na ni ajabu, lakini kote katika Biblia, Yeye kamwe hakuwa na manabii wawili, manabii wakuu wakitenda kazi wakati ule ule. Daima alikuwa na nabii mmoja, ndipo alipomalizana na huyo, alimwondoa na kumweka mwingine mahali pake.

34 Hivyo ndivyo alivyokuwa amefanya, Yeye huwabadilisha tu wajumbe, bali roho yule yule: Eliya na Elisha. Na jinsi ninavyotamani ningalikuwa na wakati wa kuliingilia usiku wa leo, kuona ya kwamba wakati Mungu alipokuwa amemwita yule nabii mzee, mchovu kutoka hudumani. . . Alikuwa amehubiri dhidi ya Yezebeli na umati wake wa kilimwengu, na—na kuwakemea akina Ahabu, na viongozi, na mashirika ya wahudumu na kila kitu mpaka akachoka, Naye Mungu alikuwa ampeleke Nyumbani. Kwa hiyo Yeye alimleta tu chini mtoni na. . .

35 Kabla hajafanya hivyo, alitaka kumtia mafuta mtu ambaye angeuchukua Ujumbe uo huo, mnaona, Ujumbe uo huo ilibidi ubaki. Kwa hiyo akashuka na kutupa vazi lake juu ya Elisha. Naye Elisha, baada ya kuvaa vazi la Eliya, hapana shaka alilirudisha, alilitupa tu juu yake, na hapana shaka alilichukua tena, kwa sababu lilianguka kutoka mabegani mwake wakati alipopaa juu.

36 Sasa, tunaona ya kwamba Elisha, Eliya alijaribu kumvunja moyo, kasema, "Wewe ngojea hapa, kwa sababu Bwana ameniita mahali pengine." Ndipo tukaona kwamba aliendа hatua tatu: kwenda Gilgali, kisha akaendelea hadi kwenye shule ya manabii, na Yeriko, kisha akashuka mpaka mtoni na kuvuka Yordani pamoja naye.

37 Na kama tukiangalia, kama tulivyohubiri Jumapili iliyopita juu ya *Ibrahimu Na Uzao Wake Baada Yake*, tuliona ya kwamba

Yeye alimpa Ibrahimu njia panda tatu: Kupitia kuhesabiwa haki, akimwita katika mlango wa 12; mlango wa 15, kupitia dhabihu ya damu ilikuwa ni utakaso; kupitia mlango wa 17, kunyonya nguvu zake kutoka mwilini Mwake, Roho Mtakatifu, kuingiza katika mwili wa Ibrahimu kumtia nguvu kwa ajili ya mwana ajaye.

38 Kama vile alivyolifanyia Kanisa, vivyo hivyo na Uzao wa Ibrahimu: kuhesabiwa haki, kupitia Luther; utakaso, kupitia Wesley; ubatizo wa Roho kupitia uamsho wa Kipentekoste. Halafu kule kuwekwa kwa Mwana, kutoa karama Kanisani, kisha akitokea katika umbo la . . . Yeye alikuwa ni Mungu katika mwili, akijidhihirisha Mwenyewe, akijua siri za moyo katika yale Sara aliyokuwa akifanya hemani nyuma Yake.

39 Jinsi ambavyo hizo njia panda, na kuyaona hayo makanisa yakija moja kwa moja mahali pale pale. Jinsi ambavyo ilimbidi kuubadilisha mwili wa Sara na Ibrahimu baadaye, baada ya ujumbe huo, wapate kumpokea mwana aliyeahidiwa. Na hivyo ndivyo amelifanyia Kanisa hili, akalipitisha kwenye jambo lile lile. Sasa, jambo linalofuata ni badiliko katika dakika moja, kufumba na kufumbua jicho, na kuondoka.

40 Nasi itabidi tuwe na mwili uliobadilishwa. Sasa, Sara na Ibrahimu katika mwili wa namna hiyo, wasingeweza kumpokea mwana aliyeahidiwa, walikuwa na umri wa miaka mia moja, ilimbidi kuubadilisha mwili wao. Sana sana, sio kuwageuza, kuwa vijana, jambo ambalo Yeye alifanya, lakini pia, kuwabadilisha, kwa sababu wamekuwa kama walivyokuwa hapo kwanza. Lakini Yeye aliubadilisha mwili wao hivi kwamba wangeweza kumpokea huyo mwana.

41 Na sasa, tunaona jambo linalofuata katika utaratibu kwa Kanisa sasa, ni mwili uliobadilishwa, sana sana, sio sisi wazee kurudi na kuwa vijana, lakini tutarudi, na tutakuwa vijana huko, hakika kabisa, ila hatuna budi kuwa na mwili uliobadilishwa tupate kumpokea Mwana, kwa sababu tutamlaki Yeye hewani. Kunyakuliwa kunakuja, kubadilishwa katika dakika moja, kufumba na kufumbua jicho.

42 Sasa, tunaona ya kwamba Mungu alimpitisha Elisha katika hatua zile zile, hatua tatu mbalimbali. Ndipo baada ya wao kuondoka humo shuleni, wakashuka kwenda Yordani, na kuvuka Yordani, basi alikuwa na sehemu maradufu ya roho ya Eliya ilikuwa juu yake (Sasa, Yesu alisema, “Mambo haya nifanyayo ninyi nanyi mtayafanya, zaidi ya haya mtayafanya, kwa kuwa Mimi naenda kwa Baba.”), ni mfano wa Kristo na Kanisa. Kristo alitwaliwa juu, ndipo Roho yeye yule aliyekuwa juu ya Kristo, akaja juu ya Kanisa Lake.

43 Sasa, ambapo Kristo angeweza tu kuwa mahali pamoja akihudumu, sasa, katika Kanisa Lake, Yeye angeweza kuwa wa ulimwengu mzima, akihudumu kote ulimwenguni. Wazieni

tu, sisi hawa hapa Chicago usiku wa leo, pamoja na Kristo, tukihudumu; huko Filadelfia, wakimhubiri Kristo; Afrika, Japani, Asia, Ulaya, kila mahali. Dakika . . . watu dakika ii hii, kote ulimwenguni, wanaponywa kwa nguvu za Mungu, watu wanampokea Roho Mtakatifu kwa dazani, dakika ii hii, mnaona, kote ulimwenguni, sehemu maradufu, Roho Yake ikimwagwa katika siku za mwisho.

44 Mara shule ya theolojia, huko juu ya mlima kutoka Yeriko, akarudi na kumwona Eliya . . . Elisha akavuka, na kuona mwujiza aliofanya, kama tu vile Eliya alivyoufanya. Mbona, wao walisema, "Roho ya Elisha . . . Eliya inakaa juu ya Elisha."

45 Halafu basi, tunaona, basi, ya kwamba watu walijua ya kwamba Roho wa Mungu alikuwa juu ya nabii huyu. Kwa hiyo wakamtaka shauri, kama asingewafanyia mwujiza fulani, kwa ajili ya jambo jema. Akasema, "Tuna mji mzuri hapa, umewekwa juu ya kilima na ma—mandhari ni mazuri na ni mahali pazuri kwa shule," na kadhalika, "kama Eliya alivyoijenga, ila maji hapa ni machungu." Nao walihitaji ninii mpya, chemchemi.

46 Na bila shaka, walikuwa wakibadilika, iliwabidi kuwa na chemchemi mpya iliyofunguliwa. Na kwa hiyo huwezi kuweka divai mpya katika viriba vikuukuu, ingevipasua, unajua. Nami nafikiri leo ni siku pia, wakati tu—tunahitaji kubadilishiwa maji. Tunahitaji chupa ya chumvi, chupa mpya ya chumvi ambayo haijawahi kuwa na kitu chochote hapo kabla.

47 Na Mungu kwa kawaida hufanya hivyo, humwinua maskini mtu fulani kutoka mahali fulani asiyejua chochote, na kutupa chupa ya chumvi kwenye maji ya kale ya kikanisa, na muda si muda mwajua, yote yamekuwa matamu tena, uamsho mwingine, Roho Mtakatifu akishuka juu ya kila mtu, wakienda kila mahali.

48 Hicho ndicho tu—tunachohitaji usiku wa leo. Hicho ndicho tunachohitaji tena, ni kipimo kingine cha chumvi, sivyo, kuyafanya maji kuwa matamu? Kumbukeni, alichukua chupa mpya kabisa, ambayo haikuwa na kitu, na kutia chumvi ndani yake. Sasa, chumvi hutia ladha kama ikigusa, bali haina budi kugusa kwanza, haina budi kufanya mguso wake.

49 Sasa, sasa, ka—katika, huko nyuma katika ulimwengu wa kisiasa, kulikuwako na badiliko kubwa pia. Kulikuwa na m—mtu jina lake Ahabu aliyekuwa amekufa, naye mwanawe, Yehoramu, akatawala mahali pake. Naye alikuwa ni kama tu, loo, nadhani baba yake, Ahabu, alikuwa amenyosha mambo machache, lakini akawa mbaya katika mengine zaidi.

50 Na kwa hiyo, hivyo karibu ndivyo ilivyo, ifanyavyo, tunapounda mfumo mpya, mbona, tunatoa vitu vichache ambavyo mfumo wa kale haukuwa navyo, na kuweka kitu fulani labda kilicho kibaya zaidi, nasi tunaendelea tu kusonga mbele namna hiyo. Lakini hivyo ndivyo ilivyokuwa imetendeka katika wakati huu.

51 Kwa hiyo, siku chache zilizopita usiku, nilizungumza juu ya Yehoshafati kuja kukutana na Ahabu, na kufanya mapatano naye, naye akaingia katika kundi baya. Sasa, ni ajabu kwamba Yehoshafati, angali ni mfalme, katika mwaka wa kumi na nane wa utawala wake, wakati Yehoramu alipopachukua mahali pa Ahabu, Yehoshafati alishuka, ama, Yehoramu alimtumainia, kwa sababu aliingia katika matatizo, naye Yehoshafati akarudi akaingia moja kwa moja tena katika kundi baya.

52 Si ni ajabu kwamba tunafanya mambo hayo? Wanaruka moja kwa moja kutoka kwenye kikaango, wakaingia motoni. Unakuta kwamba watu wataninii, kama . . . Watatoka moja kwa moja na kuanza kumtumikia Mungu, halafu basi muda si muda mwajua, watarudi moja kwa moja ulimwenguni tena, Biblia inasema, "Kama mbwa anavyoyaendea matapiko yake; na nguruwe kugaa-gaa." Naye mbwa anapaswa kujua kama hayo matapiko yalimchefua vya kutosha ku—kuyatapika mara ya kwanza, yatafanya vivyo hivyo mara ya pili.

53 Na kama dhambi ya ulimwengu itamfanya mtu kutambua ya kwamba amekosea wakati mmoja, kumfanya atubu, itafanya hivyo mara ya pili. Kwa hiyo kwa nini usikae mbali na kitu hicho kwa vyovyote vile? Kama yalikuchefua nawe ukayaondoa, kaa mbali nayo. Jiepushe na kuonekana kwenyewe kwa uovu. Nasi tunaona ya kwamba hivyo ndivyo yanavyoendelea, hata hivyo, nasi tunayo tu, kwa hiyo sikuzote tulikuwa nayo, kwa hiyo nadhani tutaendelea tu kuwa nayo.

54 Lakini ningewazia ya kwamba—ya kwamba Yehoshafati aliwazia, "Vema, nitashuka niende nione labda huyu mchungaji mpya, Yehoramu, atakuwa tofauti, atakuwa tofauti kidogo tu na vile yule mchungaji mzee alivyokuwa." Lakini tunaona ya kwamba yeye alikuwa ni mchungaji mpya kweli, bali alikuwa na mfumo ule ule wa kale, alikuwa tu ameongeza mambo mapya kwake, pia alikuwa ameongezea mipango mipya ambayo labda ule mfumo wa kale haukuwa nayo.

55 Hivyo ndivyo nafikiri tumefanya mengi sana ya hayo siku hizi, enyi marafiki. Tuna, sisi Wapentekoste, hiyo ni sehemu kubwa ya yale tumefanya, tumechukua mfumo wa kale na huku tukijaribu kuanzisha uamsho mpya, lakini muda si muda mwajua, tunageuka na kuendelea na huo uamsho mpya, kuingiza tu mfumo wa kale ndani yake tena, na hilo ndilo linalorarua kitu hicho.

56 Sasa, hapa si muda mrefu uliopita, walivunjilia mbali kitu fulani wakati uamsho ulipoanza katika milki za Kipentekoste, unaoitwa "Mvua ya Siku za Mwisho." Vema, wakahamia sehemu mbalimbali, nao wakasema, "Sisi si dhehebu," na kisha wakaja kugundua, walikuwa wamejiundia dhehebu kali kuliko hayo mengine yalivyokuwa. Mnaona, mmerudisha mfumo wa kale pamoja na m—mchungaji mpya, nao kabisa haufanyi kazi, hivyo

tu. Nao unaingiza kitu hicho chote katika mchafuko, ndipo mmechanganyikiwa kabisa.

57 Kwa hiyo hilo ndilo lililotukia hapa, Yehoshafati alishuka kwenda ku—kumwangalia mchungaji huyu mpya, Yehoramu, na kuwazia labda angechunguza mfumo wake na kuona kile alichokuwa nacho, bali ilikuwa ni ndoana tu ya kumfanya ashikwe na matatizo tena. Halafu pamoja na hayo madoido yote na kila kitu alichokuwa nacho cha kumtolea, tunaona ya kwamba aliendа, walienda siku saba bila kumtaka Bwana shauri, pasipo kujua hakika ya kwamba Mungu alikuwa katikati yao.

58 Sasa, hiyo ndiyo shida, tunaanza kwenye mambo haya, lakini hatusimami tuone kama, kweli, ni Bwana miongoni mwetu au la, kama ni namna fulani ya mhemuko, ama namna fulani ya kujichochea, ama namna fulani ya mfumo wa kipumbavu wa kitu fulani. Tunapaswa kuninii—tunapaswa kutatua hilo jambo na kuona kama ni la Mungu au la. Nafikiri hapo ndipo tunapofanyia makosa yetu.

59 Ni siku saba ambazo Kanisa limesafiri, nasi tunaona ya kwamba katika muda wa siku saba, tukichukulia tu kwamba Mungu alikuwepo, hivyo ndivyo tumefanya. Kulichukulia tu kijuu juu, "Loo, vema, tutaenda tukajiunge na kanisa, Mungu yuko ndani yake, hakuna shaka hata kidogo."

60 Chunguza uone kama Mungu yuko ndani yake au la. Yesu alisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio," ishara, maajabu, miujiza. Basi tunapoona makanisa yetu yakipoa na mambo hayo hayatendeki, inawabidi kungojea mpaka mtakapomleta mwinjilisti maalum mjini ama chochote kile, kisha mnapiga tari chache na kuchochea mhemuko mdogo, Mungu hayuko katika hilo, la.

61 Nitawaambia tunachohitaji leo ni kurudi kwenye Biblia ya kale tena, kurudi kwenye mafundisho ya mtindo wa kale ya Kipentekoste ya Biblia, kumrudia Roho Mtakatifu, kurudi kwenye nguvu za Mungu, kurudi kwenye mikutano ya maombi ya usiku kucha, ambapo wanamwonea Mungu njaa na kiu. Hilo ndilo tunalohitaji usiku wa leo katika makanisa yetu, katika ninii yetu . . . kuleta hayo katika mifumo yetu.

62 Waligundua basi kwamba safari ya siku saba hatimaye iliwafikisha jangwani. Nasi tuliona jambo lile lile, tumekuwa na nyakati saba za kanisa. Tunaishi sasa katika nyakati saba za kanisa. Tumefanya nini wakati, uamsho ulipotokea? Tuliunda mfumo na kujifanyia kundi dogo hapa ambapo "Tunaamini *hili*. Wala hatutakuwa na uhusiano wowote na kundi *hili*." Nalo kundi hili likajiundia kundi dogo, hawatakuwa na uhusiano wowote na kundi *hili* hapa. Wanaanza tu kuzozana, kugombana, huku na huku, na sasa, tunaona katikati ya hayo yote, kwamba

tumeenda yapata siku saba wala hatuna Mungu miongoni mwetu. Hiyo ni kweli.

63 Sasa, nabii alisema kutakuwa na siku ambayo haitaitwa mchana wala usiku, ingekuwa kwa namna fulani ni siku yenye utusitusi, yenye huzuni. Tumekuwa na siku kama hiyo. Tumekuwa na siku moja kwa miaka elfu mbili iliyopita, ambapo tumekuwa na mikutano na kumkubali Yesu kama Mwana wa Mungu, kama Mwokozi wetu, nasi tumemwona Mungu akitenda mambo makuu miongoni mwetu. Lakini hata hivyo, imekuwa ni muda mrefu tangu ile Nuru ya Kipentekoste.

64 Miaka elfu mbili tuliunda madhehebu, tukajenga shule kubwa, na tukawa na mifumo, na kuona hapa, katika wakati wa saba wa kanisa, tunaona ya kwamba tumekosa kitu fulani, kuna kasoro fulani. Tunaona tuliingia jangwani, na matunda yote yamekauka.

65 Hivyo ndivyo kanisa la Kipentekoste limefanya siku hizi, limejiundia dhehebu kali sana, hata yanapingana, mpaka tukakuta kwamba matunda yote yamekauka. Hatuna tena upendo, amani, furaha, uvumilivu, ushirika, ambao tunapaswa kuwa nao, kama waliokuwa nao hapo mwanzo, matunda yote yamekaukia jangwani.

66 Safari ya siku saba, bila ya kumpata Mungu halisi, aliye hai, tumeenda kombo na *itikadi* ndogondogo. Mungu alimpa Luther kuhesabiwa haki, akakimbia nako; akampa Wesley utakaso, akakimbia nao; akawaacha Wapentekoste wanene kwa lugha, nao wakakimbia nako. Mungu anataka kutuita pamoja katika umoja wa nguvu ili kuurudisha utimilifu wa Roho Mtakatifu Kanisani tena, huku karama zote za kiroho zikitenda kazi katika kila kundi la mahali hapo.

67 Naam, siku saba bila Mungu, akawaongoza hata jangwani. Ni jambo lile lile sasa, tunda Lake limekauka. Ninawazia kwamba wakati. . .walipokuwa wakipanda kilimani kutoka kwenye mabonde ya kijani kibichi na kadhalika, walianza kuona ma—mahali hapo kwa namna fulani panakauka.

68 Unajua, kila mtu anataka ujuzi wa kilele cha kilima, nao kamwe hawataki kuchukua bonde, kila mtu, kanisa la Kipentekoste, pia. Kila usiku, kama hupazi sauti, huchezi dansi, huruki juu chini, huneni kwa lugha, na kukimbia huku na huku sakafuni, ama *chochote kile*, hukuwa na mkutano wa namna yoyote. Vema, unajua ni sawa kuwa kwenye kilele cha mlima, hilo ni sawa, lakini hebu niwaambie, matunda yako yatagandia huko juu wakati wa usiku, na kipindi cha baridi kitakapokuja, utapoteza matunda yako yote.

69 Hilo ndilo lililotukia sasa, tunatilia mkazo sana matukio ya kilele cha mlima ya kucheza dansi, na kutetemeka, na kurukaruka, badala ya mikutano ya maombi ya usiku kucha, huko chini kwenye bonde la uamuzi, ambapo inakubidi kushuka

kule chini na kukutana na Mungu na kuyamwaga maisha yako kwelikweli mpaka jambo fulani litukie. Tumeacha ninii... Tumekuza matunda kule juu, lakini mgando unayaua. Hiyo ni kweli. Kila inapofikia kipindi kidogo cha baridi, huna kitu cha kutegemea. Wakati mhemuko au ninii...unapoisha, basi kupaza sauti kwote kumekwisha, kelele zinakoma, basi ninii... uko wapi? Jaribio linakuja, ndipo huwezi kulivumilia.

70 Tunachohitaji ni kushuka kwenye mahali hapo pa kusagia, huko chini kwenye bonde hilo, tukachimbue. Hiyo ni kweli kabisa. Ndipo mahali ambapo Kanisa linahitaji kuwa usiku wa leo.

71 Vema, ninaweza kuwazia walikuwa wakiona maisha ya kijani kibichi yakianza...Unasema, "Kijani kibichi?" Naam, huenda tukawa kijani kibichi bali tuna uhai kwa vyovyote vile. Hiyo...Naam.

Kila mtu anasema, "Vema, kundi hilo la wahubiri wa Kipentekoste, baadhi yao..."

72 Nilikuwa kwenye shule fulani si muda mrefu uliopita, ndipo mwanangu akawaambia wanafunzi fulani, akasema, "Vema, mimi mwenyewe nimetoka kwenye shule ya Biblia ya Kusini-mashariki."

73 Kasema, "Kama unaweza kusoma na kuandika, wewe ni bora kuliko kundi hilo *huko*." Loo, jamani! Vema, akasema, "Vema, hao ndio kundi la kishamba sana nililowahi kuona."

74 Loo, ndugu, huenda tukawa washamba, bali tuna... tunaweza kunyumbulika. Chochote ambacho si kijani kibichi, hebu kivute kidogo na utakivunja.

75 Hiyo ndiyo shida ya siku hizi na matukio ya watu wengi kupita kiasi, makavu kupita kiasi na magumu. Tunahitaji kitu kinachonyumbulika kusudi upepo ukishuka, unaweza kukipulizia, na kukirusha kote, na kukivuta kote, kukifanya kikue, kukisukumia uhai. Afadhali kidogo niwe kijani kibichi na niweze kunyumbulika kwa Roho Mtakatifu, ili niweze kujisalimisha Kwake badala ya kusimama nikipiga kelele za maombolezo, kama ibada ya mazishi, wakati anapovuma kupitia kwangu, nikisema, "Siku za miujiza zimepita. Hakuna kitu kama uponyaji wa Kiungu." Hiyo ni ibada ya mazishi.

76 Loo, hiyo miti michanga, hata hivyo, wakati inaponyumbulika na inaweza kujitolea kwa Roho, naye Roho anaanza kuwatikisa kama upepo ukienda kasi, akiwajaza kabisa na wema wa Mungu, loo, hiyo ndiyo aina ya maisha! Huenda ikawa ni kundi la washamba, bali hilo, naam, ni kundi lililo na uhai ndani yake. Hilo ni zuri. Na kama kitu chochote hakininii, ambacho hakina uhai ndani yake, kimekufa, hilo linajulikana kisayansi, kwamba kimekufa.

77 Siku saba, na ilikuwa ninii, kumbukeni, ilikuwa kwenye siku hiyo ya saba ambapo walitambua yale waliyokuwa wamefanya.

78 Nami nafikiri tumeshuka kupitia Luther, Wesley, na—na Baptisti, Presbiteri, Methodisti, na kote kote hivyo, na sasa ni katika wakati huu wa mwisho, ambapo ndio kwanza tutambue yale ambayo tumefanya. Ninaamini ni wakati huu sasa, ambapo kanisa la Kipentekoste limetambua yale limefanya. Viongozi halisi, waliojazwa na Roho, Wakristo halisi, waliojazwa na Roho wa uamsho wa Kipentekoste, wanatambua ya kwamba jambo fulani limetukia, wamepoa. Kwa sababu kila mtu anajaribu kuishi kwenye kilele cha mlima, wameondoka bila Mungu.

79 Tunachohitaji siku hizi ni kumrudia Mungu, kurudi kwenye lile tukio, turudi. Vema, ni katika saa ya saba ambapo walitambua ya kwamba walikuwa huko nje bila matunda, hakuna upendo, wakizozana, "Ninyi ni wa Umoja." Na, "Ninyi ni wa Utatu." Na—na, "Ninyi ni wa Assemblies." Na, "Ninyi ni Church of God." Na, "Ninyi ni *hiki*, *kile* ama *kinginecho*. Hatutakuwa na uhusiano wowote nanyi." Wanaitana jina moja baya na mmoja, mwingine, jina baya.

80 Nao ulimwengu unageuka na kuangalia, na kusema, "Watu hawa wana shida gani? Wote wawili wakinena kwa lugha kwenye kanisa *hili* na kutabiri, na kuendelea. *Huyu* hapa kwenye kanisa *hili*, nao wana ninii. . .Hata hawaheshimiani, hawana adabu wao kwa wao."

81 Loo, tunachohitaji leo hii ni kurudi kwenye tunda la Roho: upendo, furaha, amani, imani, uvumilivu. Mungu anaweza kutuma karama miongoni mwao nao wataiita telepathia, wataiita ibilisi, wataiita kitu kingine. Kama kanisa moja linaidhamini na hilo lingine linaichukua, ni sawa sasa. Kwa sababu *hili* lilikuwa na uhusiano fulani nayo, haifai kitu. Loo, jamani, jamani! Ni hali ya kuhuzunisha jinsi gani! Naam, bwana.

82 Tunatambua ya kwamba tunda la imani, tunda la upendo, furaha, amani, imani, uvumilivu, wema, upole, unyenyekevu, subira. Ati subira? Mbona, ni vigumu kuvumiliana kwa muda wa siku saba, saa saba, wakati mwingine si hata dakika saba. Wataruka juu na kulitoroka hilo kanisa ukisema jambo ambalo si hasa maskini nadharia yao kipenzi ilivyo. Hawana budi kuamka na kulitoroka hilo kanisa juu yake. Loo, hawawezi kutulia hata dakika moja, hawana budi kutoka humo, "Ai, hivyo sivyo Mchungaji *Nanii* asemavyo. Haleluya, si lazima nisikilize upuuzi kama huo," anatoka nje. Loo, mwenye mashaka wee! Vema. Haya basi. Endelea.

83 Lakini jambo ndilo hilo, mnaona, wamepoteza matunda yote, tunatambua hilo. Tunda la Roho limekauka, lote limekatiliwa juu, limekauka kabisa, nalo liko pale limekauka, likawa unga, tayari kupeperushwa. Ni hali mbaya *sana*!

84 Tunatambua sasa, ya kwamba madhehebu yetu makuu, yote yako sawa, hayo madhehebu, mradi tu yanamweka Mungu ndani yake, mradi tu yana tunda la Roho ndani yake, mradi tu yana upendo na fadhili, na yako tayari kushirikiana na kumsaidia ndugu huyo mwingine, haidhuru vipi, yale anayoamini, kama yeye ni ndugu na Mungu amempa Roho Mtakatifu. Mungu huwapa Roho Mtakatifu wale wanaomtii, hiyo ni kweli.

85 Kwa hiyo kama una Roho Mtakatifu, Wamethodisti wana Roho Mtakatifu, Wabaptisti wana Roho Mtakatifu, Wapresbiteri wana Roho Mtakatifu, wa Umoja wana Roho Mtakatifu, Church of God lina Roho Mtakatifu, vema, mnabishania nini? Hebu na tuungane, hebu tusonge mbele, hilo—hilo ndilo tunalohitaji. Mnaona, si hilo dhehebu, ni huo mfumo katika dhehebu hilo unaojiondoa; huyo anayefanya hivyo ni ibilisi.

86 Kwa hiyo tunaona ya kwamba ninii yetu yote. . .kujaribu kuninii. . .majengo makubwa na miradi mikubwa ya ujenzi na kadhalika, ninawazia wa—wakati jamaa hawa walipopanda juu ya mlima huu, wafalme hawa na kadhalika, wakipanda juu, waliona katika miradi yao mikubwa, mirefu, inayoongezeka ya ujenzi, walianza kuona tunda likianza kuwa dogo zaidi na zaidi, na baada ya kitambo kidogo hapakuwapo na tunda lolote kamwe.

87 Nami ninajua tumefanya hivyo, nasi tumeona jambo hilo katika wakati wetu, wakati tukiendelea mbele kwenye wakati huu wa Kipentekoste. Wakati tulipokuwa huko chini pembeni, yapata miaka arobaini iliyopita, hakuna mahali pa kwenda na kulikuwa na shimo dogo ukutani mahali fulani, na kundi la watu wakicheka, wakiwaita watakatifu wanaojibingirisha, mbona, walikuwa wa kiroho zaidi wakati huo, kuliko walivyo sasa, hiyo ni kweli.

88 Kanisa lilikuwa katika hali nzuri zaidi, kila moja ya hayo madhehebu wakati huo, kuliko yalivyo sasa, tukinena kiroho. "Loo, hakika, tunamiliki mali yenye thamani ya mamilioni ya dola." Vema, hilo halimaanishi kitu kwa Mungu. Afadhali nisiwe na hata nguo moja, kama Yohana, nijizungushie ngozi ya kondoo, na kumjua Yesu Kristo, na kujua ya kwamba moyo wangu ni mweupe na safi mbele Zake, mbona, bila shaka, kuliko kuwa na utajiri wote wa ulimwengu.

89 Lakini jambo ni kwamba, Kanisa limeondoka bila Mungu. Wameondoka bila ku-. . .nao wamekuta kwamba tunda la Roho limeondoka kanisani. Uvumilivu, baadhi yao wakiwa na hasira ya kutosha, mbona, wangepigana na msumeno unaovuma, halafu, na kunena juu ya Roho Mtakatifu, mnaona. Mbona tunda la Roho ni upendo, na furaha, uvumilivu. Ati kuteseka? Naam, yapata—yapata dakika mbili, hivyo tu, nao hao wameondoka, mnaona. Kwa hiyo uvumilivu, matunda yote yamekauka.

90 Miradi yetu mikubwa ya ujenzi imepanuka, hiyo ni kweli, mipango yetu mikuu, ya elimu ya juu imepanuka, wachungaji wetu wameelimika vizuri zaidi, loo, jamani, jamani! Tuna digrii za kila namna, na—na inahitaji *digrii* kadhaa kugandisha pia, tufikapo kule juu, yapata wakati huo, inaonekana kufikia, yapata arobaini chini ya sufuri. Loo, bwana!

91 Lakini tu—tuna hayo yote, hiyo ni kweli. Tunavyoona, tunapanda juu zaidi, lakini matunda yote na kadhalika yanaondoka, maji yote ya Uzima yanaonekana kukauka, hakuna Uzima wa Milele tena. Karibu ni kama, kama nilivyosema hivi majuzi usiku, wachungaji wana shughuli nyingi sana na watu wana shughuli nyingi sana wakibadilishana washirika, kama tu kuchukua maiti moja kutoka chumba kimoja cha maiti hadi kingine, mahali pamoja tu hadi pengine, hiyo—hiyo ni kweli. Baadhi yao wanakaangwa na wengine wanaganda, kwa hiyo hivyo karibu ndivyo ilivyofanya. Nami nilisema kupata *itikadi* ndogondogo, ambazo baada ya kitambo kidogo zinakuwa *itikadi-vita* na haya basi, mnaona.

92 Na hapo ndipo kanisa limefikia, mpaka matunda ya Roho yote yamekaukia kila mahali. Tunaliona kila mahali, mnajua hiyo ni kweli. Afadhali tujitokeze na kusema ni kweli, kwa sababu ndivyo ilivyo.

93 Nasi tunaona ya kwamba walikuwa wakifa huko nje jangwani. Ni hali ya kuchukiza jinsi gani, ambapo hiyo iliwaongoza, kuondoka bila Mungu. Loo, walichukua dira ya siku saba, loo, hakika, walimalizia vizuri. Wanaweza kuelekeza nyuma na kusema, "Sisi, sisi ni *hivi-na-hivi* na *hivi-na-hivi*." Hiyo ni kweli vya kutosha. Lakini Mungu yuko wapi? Jambo ndilo hilo. Mungu yuko wapi katika kitu hicho?

94 Tuna makanisa makubwa zaidi na minara mikubwa juu yake, misalaba mikubwa, na viti vya kifahari, nasi tunaweza kujilinganisha na yeyote wao, sisi Wapentekoste tunaweza, pesa zikiwatiririkia wowote wale, umati uliovalia nadhifu zaidi, na ndugu, Kadilaki zimeegeshwa kila mahali, lakini Mungu yuko wapi? Mungu yuko wapi?

95 Ndipo anakapokuja katikati yake, wengi wao wanasema, "Ai, usiyasikilize hayo sasa, huo—huo ni upuuzi, usi—usiujali huo." Mnaona? Visiki tu vilivyokufa, hakuna lingine. Sasa, hiyo ni kweli. Tunda lilikaukana kutoweka muda mrefu uliopita. Loo, ni saa mbaya jinsi gani tunayoishi.

96 Basi wakati huu ulipofika, muda si muda mwajua, waliishiwa na maji. Hawakuwa na maji yoyote, ndipo wakaanza kulia, "Ole, ole! Ee Mungu, umekuwa mwema sana kwetu kutupa majengo haya makubwa, lakini," wengi wao wakaanza kulia, "yako wapi Maji ya Uzima?" Wanaona ukomunisti ukiingia, wanauona ulimwengu karibu tu umefikia mwisho wake, huku manabii wakitabiri mwisho umekaribia, na

kadhalika, ndipo tunashangaa, "Kwani Maji yako wapi? Nini kimetukia?"

97 Ndipo ikatokea mtu mmoja alilia, ama, mwenye haki alilia, "Hivi hakuna nabii mahali fulani tungeweza kumtembelea? Hivi hakuna nabii mahali fulani?" Yehoshafati mwenye haki akapaza sauti, "Je, hakuna nabii? Tuko katika hali ya hatari. Hivi hakuna mtu mahali fulani ambaye tungeweza kumtaka shauri kuhusu jambo hili?"

98 Sasa, kama madhehebu yetu yametufikisha mahali tulipo kwa sababu tumejitenga mmoja na mwingine, tukionekana hatuna imani, basi hapana budi kuwe na kitu fulani mahali fulani. Sasa, wenye haki wanalia, "Yuko wapi mtu huyo wa Mungu? Yuko wapi mtu huyo, anayeweza kutwambia?"

99 Yeye yupo hapa usiku wa leo katika Utu wa Roho Mtakatifu. Yeye Ndiye anayeweza kuwaambia la kufanya, Yeye Ndiye anayeweza kuichoma mioyo yenu, Yeye Ndiye anayeweza kuzifunua dhambi zenu, Yeye Ndiye anayeweza kukuondolea shaka, na *kutumaini ndivyo* na kuleta *kujua hivyo* ndani yako. Yeye Ndiye anayeweza kufanya jambo hilo, Utu huo wa Mungu unaitwa Roho Mtakatifu, Yeye Ndiye aliyepo.

100 Sasa, tunaona ya kwamba wote walianza kupaza sauti, na kuona kwamba matunda yote yalikuwa yamekwisha, yalikuwa yamenyauka, nao walikuwa hawana maji. Na—nao, huyo mtu mwenye haki, bila shaka, yule mteule akasema, "Je, hakuna, mahali fulani, nabii ambaye tungemtaka shauri? Hivi hakuna mtu ambaye tungeweza kumshika anayejua jinsi ya kututoa katika hali hii, mtu ambaye si wa mchanganyiko wetu hapa? Sote tumeingia hapa, tukafanya muungano, nasi tukakusanyika hapa juu ya kilima, nasi tunaenda vitani, nawe utaona kwamba hatuna ninii, hatuna kitu cha kupigana nacho."

101 Hiyo ndiyo shida ya kanisa siku hizi, tuna washiriki wengi sana, wote wamekufa; tuna madhehebu mengi makubwa mno, yamekufa; tuna shauku nyingi sana, lakini ziko katika njia mbaya: ni nani anayeweza kuvalia vizuri zaidi, na ni nani anayeweza kuwa mbele zaidi, na ni nani aliye na shule bora zaidi, inayoweza kushinda timu nyingi zaidi za mpira, ama kucheza karata iliyo bora zaidi, ama kitu kama hicho.

102 Tunataka Mungu, si moja ya mambo hayo. Mrudieni Mungu tena.

103 "Yuko wapi? Hivi hakuna nabii mahali fulani anayeweza kutwambia la kufanya? Hivi hakuna mtu ambaye tungeweza kumtaka shauri?" Loo, ni hali ya jinsi gani! Hicho kilikuwa ndicho kilio cha mwenye haki, kulikuwa na mmoja tu miongoni mwao, huyo alikuwa ni Yehoshafati, alikuwa ni mtu mzuri, bali aliingia katika kundi baya.

104 Hiyo ndiyo shida usiku wa leo, watu wengi sana wazuri, watu wengi wazuri, huko nje katika madhehebu hayo yote huko

nje, kote kila mahali, watu wazuri, bali tunakabiliwa na ukweli fulani, tunakabiliwa na jambo fulani, kwamba ambapo Uislamu na Ubudha na itikadi zingine zinaweza kutoa saikolojia nyingi kadiri kanisa la Kikristo linavyoweza kutoa. Hiyo ni kweli.

105 Tunachohitaji si mwenendo wa saikolojia, si mwenendo wa theolojia, bali tunahitaji mwenendo wa Roho Mtakatifu Kanisani, mpaka watu wapaze sauti, "Yuko wapi yule Mungu aliyeishi wakati mmoja? Yuko wapi yule Mungu wa Pentekoste? Yuko wapi yule Mungu ambaye huchukua moyo wa mwenye dhambi na kuusafisha ukawa mweupe kama theluji, Anayemchukua kahaba kutoka mtaani, akamfanya mama wa heshima, anamchukua mlevi kutoka kwenye baa huko nje, na kumfanya mhubiri? Yuko wapi Mungu huyo anayeweza kutoka na kuichukua miguu hiyo iliyolemaa na kuinyosha, kuyafanya hayo macho mapofu kuona, hayo masikio kiziwi yasikie, kuifanya kansa hiyo itoweke? Yuko wapi yule Mungu aliyefanya hivyo wakati mmoja?" Jambo ndilo hilo. Tulikuta kwamba kuna kasoro fulani.

106 Hivi majuzi usiku nilipokuwa nikihubiri juu ya somo la *Taarifa ya Habari*, *Iliyo Kuu Kuliko Zote Katika Historia*, maskini Yohana, macho yake yalininii, nabii Yohana, kidogo yaliingia utando. Alikuwa kama, alikuwa na roho ya Eliya, naye Eliya alichanganyikiwa alipokuwa chini ya mretemu, Yohana alichaganyikiwa gerezani. Naye alikuwa ni nabii mwenye sauti kali sana, hizo hali za kuhangaika, na ndipo jicho lake la tai likaingia utando, akasema, "Nendeni muone kama nilikosea. Mwulizeni kama Yeye Ndiye, ama, Ndiye, ama tumtazamie mwingine?"

107 Yesu kamwe hakumtumia kitabu chochote, "Sasa, hiki hapa *Jinsi ya Kuwa Na Subira Ukiwa Gerezani*," ama kadhalika. Yeye alisema nini? Alimwambia nini? Alisema, "Kaeni tu na mtazame mkutano wa alasiri ya leo kisha mwende mkamwonyeshe Yohana: Viwete wanatembea, vipofu wanaona, ninii . . . "

108 Yohana alikuwa amehubiri Injili ya kwamba Masihi yuaja ambaye ange-. . . pepeto mkononi Mwake, na angeisafisha sakafu kabisa, hakika, angeyateketeza makapi kwa Moto usiozimika. Lakini wakati alipokuja, alikuwa ni Jamaa mdogo, mpole, mpole na mnyenyekevu, haiku—haikukidhi jinsi Yohana alivyodhani inapaswa kuwa.

Lakini Yeye alisema, "Nendeni mkamwambie Yohana niko moja kwa moja kwenye wakati uliokusudiwa, ni sawa, kila kitu ni shwari."

109 Ndivyo ilivyo usiku wa leo, kanisa, watu wa ulimwengu wamekuwa wakitarajia Methodisti, Baptisti, Presbiteri, ama kanisa fulani kuweka kitu fulani cha kumrudisha Kristo, Yeye yuko kwenye wakati unaofaa kabisa: Viwete wanatembea, vipofu wanaona, viziwi wanasikia. Utukufu! Yuko moja kwa

moja kwenye wakati uliokusudiwa. Amina. Hakuna kitu kibaya, Yeye anaendelea moja kwa moja. Mungu angali anaishi, Yeye angali ni Mungu.

110 Ndipo mtu huyu mwenye haki akapaza sauti, "Loo, hivi hakuna nabii mahali fulani ambaye tungemtaka shauri?"

Sasa, kuna ndugu mmoja mzuri miongoni mwao, nami ninaweza kumsikia akisema, "Naam, naam, na—namjua mtu kama huyo, na—namjua mtu kama huyo."

111 Ninaweza tu kumwona akigeuka kumtazama Yehoramu, na kusema, "Sasa, hutamwamini, ninajua tu ya kwamba sasa hivi, hutamwamini jamaa huyu, kwa sababu baba yako hakumwamini. Hakika hakumwamini. Naye baba yako alikuwa na shule hiyo huko juu ya kile kilima cha lile kundi la manabii kule juu, ama *wanavyojiita*, nao hawakumwamini. Mbona, walisema ninii . . . Naye mtu huyu nimjuaye, Roho ya baba yake iko juu yake. Anafanya jambo lile lile analofanya baba yake, alifanya jambo lile lile alilofanya Eliya. Nayo roho ya Eliya inakaa juu ya Elisha, nami nimekuwa kwenye mikutano yake, nami ninajua ni kweli." Amina.

112 Mungu atusaidie. Hilo ndilo tunalotaka, mikutano kama hiyo, ambapo tunamwona Roho wa Baba yetu, Yesu Kristo, ambaye alikuwa ninii, Eliya alikuwa ni mfano. Mnaona, Roho, "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya." Loo, ndugu, Huyo Ndiye.

113 Ndugu huyu mwema akasema, "Ninajua mahali mtu huyu alipo. Ni—nimeiona roho ya Eliya juu yake, alimwaga maji mikononi mwake, aliishi pamoja naye, nami ninajua ya kwamba roho ya Eliya iko juu ya Elisha, najua. Yehoramu," kasema, "usingeweza kuamini hilo. Wala shule yenu yote ya manabii huko nyuma pia wasingeamini hilo, seminari yenu ya kitheolojia, kwa sababu nitawaambia ni kwa nini, hii hapa sababu: Wakati Elisha aliporudi na kuwaambia ya kwamba Eliya alikuwa ametwaliwa juu, naye alikuwa na sehemu maradufu yake, mbona, walisema, 'Huyo mtu amerukwa na akili. Undeni kundi la yapata watu hamsini mwone kama alitwaliwa. Ha—hakutwaliwa kamwe, angali yuko huko nje mahali fulani.' Nao . . . "

114 Tumejaribu mifumo yetu yote ya kikanisa, loo, msinikasirikie, lakini hebu niwaambie, mifumo hii ya kikanisa imechukua zaidi ya miaka elfu mbili kujaribu kumpata Bwana Yesu aliyeinuliwa kupitia mipango ya elimu, kupitia theolojia, na kupitia madhehebu ya kanisa, nao wameshindwa kumwona. Amina. Yeye haji kupitia theolojia ya kujibunia, haji kupitia madhehebu, Yeye huja kupitia kwa moyo uliosalimishwa, kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu moyoni. Amina. Mifumo yetu ya kujibunia haimwoni Yeye.

115 Loo, waliunda makundi wakaenda na kumtafuta, kasema, "Loo, la, Roho kamwe hakumtwaa mtu huyo. Sasa iweni watu wenye busara, mnajua sote tuna Shahada yetu ya Sanaa, na kadhalika, kwa hiyo tu—tunajua vizuri zaidi kuliko kitu kama hicho. M—mtu aliyeketi hapa, na kula ugali wa mahindi pamoja nasi, na kadhalika? Mbona, tunajua ya kwamba mtu huyo hangalitwaliwa katika gari la Moto. Mvulana huyo amesisimkwa kabisa sasa, amekuwa upande wa pili kule, naye amerudi akiwa na ushupavu mwingi wa dini, kwa hiyo tu—tunajua vizuri zaidi ya hayo. Kwa hiyo mketisheni tu huyo mzee chini, upara wa—wake umeshikwa na joto sana, mwajua, na kwa hiyo yeye... hebu na tumpepee tu kidogo. Ninyi nyote nendeni kule mwone ni kitu gani kimetukia kule. Tafuteni, watumeni makundi kadhaa."

Kasema, "Nendeni, ila hamtampata."

116 Nidhihakini, niiteni *baradhuli* mkitaka, lakini Mungu ameninii...kamwe hamtampata katika mifumo yenu ya kimadhehebu. La, bwana. Yeye alitwaliwa juu, Naye anakuja tena katika mfano wa ubatizo wa Roho Mtakatifu. Wala kamwe hatawaelimisha watu kwake, hawana budi kuzaliwa ndani yake, hawana budi kuwa na ubatizo wa Roho Mtakatifu, hakuna chochote pungufu.

117 Sio kujichochea kiakili, mhemuko fulani, au mfumo wa kikanisa, wala ishara, bali haina budi kuwa ni Roho Mtakatifu halisi, wa kweli anayeleta tunda la Roho wa upendo, furaha, imani, uvumilivu, wema, upole, subira. Jambo ndilo hilo, jambo ndilo hilo. Naam.

118 Hakika Yehoramu asingeweza kufanya hivyo, asingeamini hilo. Yeye, mnaona, hawangeweza kuamini hilo, ile shule ilisema, "Sasa, ngojeni kidogo hapa, sasa, tunajua jamaa huyu kwa namna fulani amesisimkwa kupindukia, kwa hiyo tutamwacha aketi hapa, nasi tutayakusanya makundi yetu pamoja tuondoke kwenda kumchukua tena, yuko huko nje mahali fulani."

119 Na hivyo ndivyo tumejaribu kufanya kwa miaka elfu mbili. Nanyi Wapentekoste, mnafanya jambo lile lile, mkijaribu kumchukua kwa madhehebu. Kamwe hamtafanya hivyo, kujitenga na ndugu wengine, hamna budi kurudi, na hatuna budi kuwa mmoja, Sijali kama mtu huyo amekosea. Kama amekosea na ni mwaminifu moyoni mwake, nawe uko sawa katika imani yako na—nawe umekosea katika kutenda jinsi unavyotenda, afadhali niwe mahali pake kuliko kuwa mahali pako. Hiyo ni kweli. Afadhali nikosee katika fundisho langu, na niwe sawa moyoni mwangu, Mungu ataliheshimu zaidi.

120 Kwa hiyo kama mtu amekosea, vipi kuhusu hilo? Msaidie, anahitaji usaidizi, mpende. Kama huwezi kumpenda adui yako kama vile unavyowapenda wale wanaokupenda, wewe si bora kuliko watoza ushuru. Sawa. Hilo ndilo kanisa limeshindwa kupata. Natumaini mnalipata usiku wa leo, natumaini mnaona

kile ninachozungumzia. Ni kurudi kwenye upendo, upendo wa ukombozi, mambo mengine yote ni sawa, lakini hatuna budi kurudi kwenye ushirika sisi kwa sisi.

121 Nao watu wanasema ya kwamba ninayashambulia madhehebu, siyashambulii, ninashambulia mfumo huo humo ndani ambao unavunja udugu, daima nimefanya hivyo, na daima nitafanya hivyo, hiyo ni kweli, kitu hicho kinachotenganisha udugu. Hebu tuje pamoja, hebu tuwe ndugu.

122 Kama ningeweza kuona kila kanisa katika mji huu, kila kanisa ulimwenguni likija kama tulivyokuwa hivi majuzi asubuhi kwenye kile kiamshakinywa cha wahudumu, nilipoona wa Umoja, Uwili, Utatu na wote, wakikumbatiana, wakikumbatiana kwa mikono yao, Ningesema, kama Simeoni wa kale, "Bwana, mruhusu mtumishi Wako aondoke kwa amani, kwa kuwa macho yangu yameuona wokovu Wako." Hiyo ni kweli.

123 Unaweza kulifafanua katika jamii ndogo, na halafu muda si muda wajua, ibilisi atarudi mle ndani, alisambaratishe tena. Halafu unaweza. . . Lakini kote ni, huwezi kufanya hivyo. Itatendeka siku moja, Mungu atawatumia a—adhabu nao itawabidi kufanya hivyo.

124 Kwa hiyo Askofu Yehoramu, kamwe asingeamini hilo. Alijua asingeweza kuliamini, maana baba zake hawakuliamini. Hakuamini ya kwamba Eliya alitwaliwa juu, kwa hiyo ataaminije jambo hili? Kupitia theolojia isiyo na maana, wangetafuta.

125 "Sasa, sisi ni shule ya manabii, tumeyaandaa yote, tunajua yale hasa Yeye anayopaswa kufanya, tunajua jinsi hasa anavyopaswa kufanya, tunajua jinsi anavyopaswa kuenenda, tunajua ya kwamba jambo pekee unalopaswa kufanya ni kuingia na kusema, 'Ni—ninaamini,' na kupeana mikono, nasi tutanyunyizia *hivi* ama kubatiza *hivi*, ama nyuma *hivi* ama nje *vile*, ama," loo, jamani, "nasi tumelipata." Sasa, hivyo ndivyo tu afanyavyo.

126 Nanyi mnaendelea na kubatiza *hivi* na kubatiza *vile*, na kunyunyizia *hivi* na kunyunyizia *vile*, na kupokea ushirika *hivi* na *vile*, nanyi mngali mnakuta kwamba hamna Mungu. Mna namna ya taratibu za dini, hivyo tu. "Mungu ni Roho, nao wamwabuduo imewapasa kumwabudu katika Roho na kweli." Amina. Mungu tututumie manabii tena kukirarua kitu hicho, na kuleta kweli itakayoonyesha jambo hilo. Theolojia isiyo na maana. Loo, jamani!

127 Sasa, tunaona ya kwamba yeye alisema, "Naam, ninajua mahali mtu huyu alipo."

128 "Tutashuka tu na. . . " Vema, wao, vema, bila shaka, huenda baadhi yao walishangazwa na jambo hilo. Lakini—lakini mnaona hapa, ya kwamba Yehoshafati, yule mtumishi wa kweli,

mteule wa Mungu, kasema, "Roho wa Mungu yuko juu yake." Naam, bwana.

129 Akasema, jamaa huyu alisema, "Ninajua alipo Elisha," kasema, "alimimina maji juu ya mikono ya Eliya, Mtishbi. Yeye ali-. . .roho ya—ya Elisha iko juu, uh, ya Eliya iko juu ya Elisha. Sasa, ninajua ya kwamba ana roho yeye yule, kwa hiyo basi . . . "

130 Na mara mtu huyo wa Mungu aliposikia ya kwamba roho ya Eliya ilikuwa juu ya mtu mwingine, naye mtu huyu alikuwa akifanya jambo lile lile ambalo Eliya alifanya, alijua huyo alikuwa ni nabii halisi. Naye alijua kama roho halisi ya Eliya ilikuwa juu ya mtu mwingine, angefanya jambo lile lile ambalo Eliya alifanya.

131 Na hebu niwaambieni ndugu zangu, hebu niwaambieni rafiki zangu, wakati Roho wa Yesu Kristo atakapokuja juu ya Kanisa, Kanisa litafanya jambo lile lile alilofanya Yesu Kristo, I—I—Itafanya: "Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya." Naye alithibitisha hilo, alisema wangefanya hivyo, kama hawatafanya hivyo, vema basi, kuna kasoro mahali fulani. Wanamfanya tu Mungu kusema uongo, kama wakisema wao ni mwaminio na mambo haya hayatendeki. Naye alisema neno la kila mtu na liwe uongo na Lake liwe kweli.

132 Kwa hiyo tunaona ya kwamba alisema, mtu huyu alisema, "Roho wa yule nabii halisi, wa kweli, anakaa juu yake."

133 Ndipo mara tu, huyu mteule, anayewakilisha Kanisa teule la siku hizi, lililoteuliwa na Mungu kwa ajili ya siku hii ya mwisho, alisema, "Basi tutaenda kumsikiliza kwa sababu Roho wa Mungu yuko juu yake." Loo, napenda hilo! "Maadamu tunayaona mambo hayo ambayo Eliya alifanya yako juu ya mtu huyu, tutaenda kumsikiliza."

134 Ndugu huyu mwema alisema, "Vema, nimetoka nje siku nyingi usiku na nimemsikia, nami ninajua hii ni kweli, kwa hiyo twendeni tu kule tukamwite."

135 Kwa hiyo walipokuja mbele ya nabii, loo, jamani, ni—ni ugomvi wa jinsi gani alioingia! Huenda hili kwa namna fulani likadhuru utakaso wake kidogo, bali kweli alichemka kabisa, alimwambia Yehoramu, akasema, "Kwa nini usiende kwa manabii wako mwenyewe?" Jamani! "Kwa nini usimwendee nabii wa mama yako? Kwa nini usiende kwa manabii wa baba yako? Nenda kwa watu wenu baridi sasa, ukajiunge nao ukitaka. Uko kwenye matatizo, mbona usiwaendee?"

136 "Loo, la, la," akasema, "lakini Bwana ametuleta huku nje." Kasema, "Tuta—tuta—tutakufa. Tutauawa kwa kuwa . . . "

137 Mnaona, sio kwamba tu mtakufa, tayari wamekufa, matunda yote yamekauka, na Roho yote imetoka kanisani, tayari limekuwa tu dhe—dhehebu la kidini. Hiyo ni kweli. Kuna kasoro.

Kama hatuwezi kumrudisha Mungu kanisani mahali fulani, tutafanyaje? Basi sote tutaangamia.

138 Na wakati nabii huyu, baada ya kumaliza kumkemea, alisema, "Kama si kwamba niliheshimu uwepo wa Yehoshafati, yule mteule, hata nisingekuangalia." Loo!

139 Nafikiri hivyo ndivyo Mungu angesema usiku wa leo. Kama haikuwa...Ninyi watu ambao mmejifunga wenyewe kwa madhehebu haya mbalimbali na kuzozana, kama haikuwa kwamba Mungu alikuwa anawaheshimu watu ambao kweli walimwamini, kamwe hakungekuwako na Oral Roberts, ama chochote kilichotumwa kote nchini, kamwe kusingekuwako na ishara na maajabu. Hata asingetuangalia kama haikuwa...Sisi sote tuna hatia.

140 Kama haikuwa kwa ajili ya Wateule, kama haikuwa kwa ajili ya Kanisa, wale ambao kweli wanamwamini Mungu, hata asingetuangalia. Hiyo ni kweli. Lakini kwa sababu kuna watu wanaotaka kuamini, Mungu ana mjumbe kwa ajili yao. Amina. Roho Mtakatifu angehuzunika akaondoka muda mrefu uliopita.

141 Maskini nabii huyu kweli alishikwa na hasira yake ya haki, naye akawakemea, naye akawaambia kuhusu miungano hii yote na madhehebu waliyokuwa nayo. Akasema, "Hata hivyo," kasema, "nileteeni mpiga kinanda." Loo, ilimbidi kupunguza hasira yake kidogo, mwajua, alikuwa amechemka sana, na kwa hiyo akasema, "Nileteeni mpiga kinanda."

142 Sasa, vipi kuhusu baadhi yenu ninyi watu wa Church of Christ, *mnavyojiita*, ambao hamuamini katika muziki kanisani? Baada ya kuchemka sana, alihitaji muziki kidogo kumshushia Roho. Hiyo ni kweli. Naam, bwana. Na, sasa kumbukeni, Mungu habadiliki, na kama muziki mzuri ulimleta Roho juu ya huyo nabii wakati huo, utafanya jambo lile lile leo. Hiyo ni kweli kabisa, maana Mungu anaupenda. Hakika.

143 Akasema, "Nileteeni mpiga kinanda." Vema, unasema, "Vema, naam, mimi siye yule nabii." Lakini labda unaweza kuwa sehemu ya mpiga kinanda, wajua, u—unaweza kufanya jambo fulani kwake, hivyo tu. U—una ushuhuda ama jambo fulani unaloweza kufanya.

144 Ninaweza kuwaona wakimleta mpiga kinanda na kucheza, "Mambo yote yanawezekana, amini tu," na kumrudisha Roho, akaanza tena. "Amini tu, amini tu, mambo yote yanawezekana," ilibidi kucheza kidogo kabla Roho hajamjia huyo nabii. Ndipo wakati nabii alipokuja, akaona, wakati Roho alipomjilia nabii, hasa, aliona ono.

145 Sasa, hivyo ndivyo, mnaona, asingeweza kufanya hivyo... Kundi kubwa la watu wenye elimu, walioteuliwa, kundi le—lenye vyeo vikubwa, wafalme, na watawala, kwa upande wa kiakili, kielimu, wasingeweza kuona lile ono, hiyo ni kweli, walikuwa vipofu.

146 Hiyo ndiyo sababu, usiku wa leo, wanataka kuliita ono la Mungu wendawazimu, telepathia, roho ya ibilisi ama kitu fulani, ni kwa sababu wao ni wenye akili sana, hawajui chochote kumhusu Mungu, hiyo ni kweli.

147 Lilikuwa ni ono lililosema kweli, huo ulikuwa ni mpango wa Mungu, hiyo ilikuwa ni njia ya Mungu, kwa sababu Roho wa Bwana alikuwa juu ya nabii, nalo Neno la Bwana lilimjia nabii. Naam, bwana. Nalo lilikuja vipi? Kupitia ono. Naam, bwana. Lilikuja kupitia ono, sio kwa njia ya kiakili, ilikuwa imeshindwa. Na ndivyo imefanya sasa.

148 Ndipo akachukua, akaangalia na kuona ono, akawaza, "Mbona, hili ndilo," Roho wa ujumbe. Sasa, aliona nini? Sasa, hivi yeye alisema tu, "Loo, Yehoramu, unahitaji digrii nyingine. Nami nakwambia, Yehoshafati, umepata matatizo kidogo, kwa hiyo unapaswa kuondoka na kusoma kwa muda kidogo zaidi, kwa sababu nakwambia, kweli hujui jinsi ya—ya kufanya mambo haya, hujui jinsi ya kuliongoza jeshi," ama kitu fulani? Haikuwa hivyo, hakufanya hivyo.

149 Alisema, "Hebu nikwambie unalopaswa kufanya, unapaswa kuwaadibisha wanaume wenu, hawavai sare zinazofaa, hivyo ndivyo ilivyo. Mnapaswa kuwafanya makasisi wenu wote waupindue ukosi wao, ili waonekane kama kasisi, mnaona."

150 Loo, litakuwa katika Pentekoste hivi karibuni sana, naam, litakuwa hivi karibuni, moja kwa moja ndani yake. Lina-. . .Kanisa Katoliki lilikuwa ndilo kanisa la kwanza la Kipentekoste, kumbukeni. Hiyo ni kweli kabisa. Sasa, ninyi, baadhi yenu wanahistoria mnakanusha jambo hilo. Hebu ipeni Pentekoste miaka mingine mia moja na hamsini, itakuwa mbali zaidi kuliko kanisa la Kipentekoste lilivyo, kwa kiwango wanachoendea sasa. Hiyo ni kweli.

151 Loo, naam, kanisa Katoliki lilianzia Pentekoste, kisha wakaliundia madhehebu na wakaingiza mashirika makubwa mle ndani yaliyotaka kufanya *hivi* na *vile*, ndipo Wanikolai wakawashinda walei na kuondoa ninii—na kuondoa mamlaka kutoka kwa walei huko nje. Roho Mtakatifu hawezi kuja *huko* nje, yote yanapaswa kuwa *hapa*, yale jamaa mmoja asemayo, ni hayo tu. Roho Mtakatifu anakaa katika Mwili wote wa Kristo. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . .Roho Mtakatifu akiliongoza kanisa, mbona, waliyakausha matunda yote, nanyi mnaona mahali lilipo sasa. Vema, Pentekoste iliingia kwenye mkondo uo huo, moja kwa moja kwenye njia ile ile, kwa hiyo haya basi.

152 Sasa, tunaona wakati Roho alimjia, ni ono gani la—la Roho alilompa nabii? Alisema nini? Hakusema, "Sasa, watoe askari wako wote nje ukawasomeshe tena, ili kwamba watakapoenda juu ya kilele cha mlima, watajua zaidi la kufanya, ukawafundishe theolojia zaidi. Wanapaswa kuadibika kidogo,

wanapaswa kubeba kisu kirefu zaidi," ama kitu kama hicho, ama, "wanapaswa kuvaa sare tofauti." La, hakusema hivyo.

153 Alisema, "Anzeni kuchimba. Njoni huku kwenye jangwa hili, watu wenu wakati mmoja walivuka jangwa hili, nao walitaka the—theolojia juu ya Mlima Sinai." Mungu aliwapa hiyo baada ya neema kuwapa na—nabii, na—na Nguzo ya Moto na kila kitu, bali walitaka kitu kilichowabidi kubishania, kwa hiyo akawaacha wakae huko nje nyikani mpaka wapiganaji wa kale wote wakafa.

154 Akasema, "Walikuwa huko nje wakati mmoja, wakiangamia vile vile mnavyoangamia. Sasa, kuna njia huko nje, kuna njia nyingi sana ambapo Mwamba huo ungali uko nyikani kule, lakini," kasema, "huna budi kuchimbua vitu vingi sana."

155 Hilo ndilo ono usiku wa leo, ndugu, sio kuanzisha dhehebu jipya, ni kuchimbua kilicho ndani yake. Hiyo ni kweli. Jambo la kwanza hilo gogo la kale la madhehebu, lililooza, litupe kando ya njia. Njia za baraka za Mungu zote zimezibwa usiku wa leo, magogo ya madhehebu yamewekwa ndani yake. Halafu gogo lingine limewekwa huko nje liitwalo—liitwalo, "Hakuna kitu kama Roho Mtakatifu," kama ukichimba chini na kuligonga gogo hilo, litupe nje. "Hakuna kitu kama ubatizo wa Roho Mtakatifu, huo ni kwa ajili ya wanafunzi tu," lichimbue.

156 "Roho Mtakatifu alikuwa tu kwa ajili ya wale mitume." Dk. Simoni Petro alisema, kwenye Siku ya Pentekoste, "Ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, kwa wale walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie."

157 Ndugu mashuhuri, mzuri Mpentekoste aliniambia, si muda mrefu uliopita, kasema, "Hatuhitaji uponyaji mwingine wa Kiungu, hata nisingeruhusu ufanyike kanisani mwangu." Akasema, "Tuna madaktari wazuri na kadhalika siku hizi, wanaochukua mahali pa huo." Hmm, hmm, hmm! Mnaona kile—mnona ni maskini gogo la aina gani linaloingia mle? Inafanya nini? Inazuia mtiririko wa maji.

158 Ono la Elisha lilimwonyesha kwamba huko nje nyikani, papo hapo ambapo matunda yalikaukia, usianzishe shirika jipya, mvua nyingine ama chochote kile, safisha tu hiyo mifereji ambapo mvua ya kwanza inaweza kutiririkia, maji yapo, Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Nao huo Mwamba uliopigwa ulikuwa nyikani, na ungali upo usiku wa leo, Mungu ashukuriwe.

159 Yesu aliwasafishia tena pale Kalvari, lakini wakarudi moja kwa moja, wakatupa magogo ndani tena, wakayazuia yote. . . Mnajua inavyofanya kutupa gogo kwenye mkondo, kitu gani kinachofanya hivyo. Vema basi, kila namna ya uchafu hulipiga gogo hili na kuliosha, na muda si muda mwajua, maji yote yanazuiliwa, kama vile panyabuku wafanyavyo, na kujenga bwawa, wala huna kitu cha kupitia humo. Hiyo ni kweli.

160 Tuna wahubiri panyabuku wengi kupita kiasi siku hizi, wakijaribu kuyazuilia maji yote, na kusema, "*Hili* ni letu, *hili* ni letu tu sisi hapa, *hili* ni mali yetu." Na inakuwaje kwake? Yanatuama. Hiyo ndiyo shida na mengi ya madhehebu yetu, kujaribu kuyazuilia maji kwa ajili ya madhehebu yenu tu, yametuama.

161 Unajua maji yaliyotuama huwa na maskini vifurukuta mikia hawa ndani yake. Hiyo ndiyo shida ya kanisa siku hizi, kufurukuta kidogo *hapa* ndani na kufurukuta *huko* nje. Kila kitu. . . "Siku za miujiza zimepita. Hakuna kitu kama uponyaji wa Kiungu." Huwezi kuketi kimya kwa dakika tano kwenye mkutano. Loo, jamani! Maji yaliyotuama, mabwawa ya panyabuku, yalipueni. Amina.

> Kuna Chemchemi iliyojaa Damu,
> Iliyotolewa kwenye mishipa ya Imanueli,
> Ambapo wenye dhambi wakitumbukia chini
> ya hiyo gharika,
> Wanapoteza madoa yao yote ya hatia.

162 Nabii alisema, "Shuka uende kule ukachimbue magogo hayo yote."

"Vema, nakwambia basi, Nabii, je, hivi turudi nyuma na kupata upepo mwingine wenye nguvu ukienda kasi?"

"La."

"Tuanzishe mvua nyingine ya vuli?"

"La, la. Safisheni tu huo mfereji, hivyo tu ndivyo mnavyopaswa kufanya."

163 Tuna watu, usafisheni tu huo mfereji. Hao watu wako sawa, safisheni tu hiyo mifereji kusudi Roho Mtakatifu aweze kuingia. Ulokole wenu wote, na itikadi, na kila kitu kingine kilichoko kanisani, safisheni kitu hicho. Mwamba tayari umepigwa, maji ni safi, yanatiririka, lakini mifumo yetu ya kikanisa imevifunga vijito.

164 Akasema, "Safisheni vitu hivyo. Haitakubidi kuwa na upepo mwingine unaoenda kasi. Hutasikia upepo wala hutaona mvua yoyote, bali hata hivyo kutakuwako na maji kule." Loo, ndugu! Si mfumo mpya, si mfumo mpya tunaohitaji, tunachohitaji ni kusafisha mfumo tulio nao. Sio kuunda Assemblies of God nyingine, ama Umoja mwingine, bali kusafisha tu Umoja na Assemblies tuliyo nayo.

165 Kuondolea mbali magogo yote, tofauti zote, ugomvi na ubishi, na vitu kama hivyo mbali nayo, maji yataanza kutiririka tena. Kutakuwako na upendo, furaha, furaha kama mto, vikitiririka tu kote juu ya kila mtu, kwa kupendana tu mmoja kwa mwingine.

> Hatujagawanyika,
> Sisi sote ni mwili mmoja;

Mmoja katika tumaini na Mafundisho,
Mmoja katika upendo.

166 Jambo ndilo hilo, mnaona. Hivyo ndivyo hatuna budi kulifanya. Hilo ndilo wazo. Hilo ndilo ono la siku hizi. Hilo lilikuwa, hilo lilikuwa ndilo ono la nabii *huyo*. Nabii wa kweli ana ono lile lile leo. Si ninii jipya—si dhehebu jipya, kuanzisha kitu fulani na kuunda kundi lingine, ungelibishania tu na kuliundia dhehebu na kulifanya tu kama hayo mengine, ungetupa magogo ndani yake pia.

167 Nilipoingia hudumani kwa mara ya kwanza, wengi wao walinijia, na kusema, "Vema, Ndugu Branham, unapaswa kuanzisha dhehebu dogo."

168 Nikasema, "Ati dhehebu? Sisi—sisi ni...Hilo ndilo ninalopinga." Nikasema, "Tunachohitaji si madhehebu, bali kusafisha kitu tulicho nacho." Hiyo ni kweli, kukisafisha. Tunahitaji uamsho, kile tunachohitaji, wakati wa kuchimba. Chimba, chimba, kadiri unavyochimba chini zaidi, ndivyo utakavyopata maji mengi. Kama ukichimba chini, useme, "Vema, nitatoka tu kwenye madhehebu," angalia vitu ambavyo ungali navyo mle ndani, kijicho, ugomvi, kila kitu kingine, safisheni hiyo mitaro mpaka mfikie moja kwa moja kwenye mwamba imara. Hiyo ni kweli. Shukeni chini mpaka ambapo maji kweli yanaweza kutoka kwenye mishipa ya Imanueli. Ngojeni mpaka mtakapofika mahali hapo, kutakuwako na maji yakibubujika tu kama chemchemi, kutoka, yakitoka.

169 "Chimbeni mitaro hii yote." Akasema, "Shukeni huku chini katika mabonde haya. Ninyi jamaa ambao mmekuwa mkijaribu, kuishi juu ya paa la nyumba huko juu wakati wote, juu mlimani, mkipaza sauti, na kuruka, na kuganda, na kukaanga, na kadhalika," kasema, "vema, msifanye hivyo, shukeni hapa chini na kuchimba mitaro hii chini hapa na kuchota maji safi." Hilo ndilo tunalohitaji.

170 Shukeni hapa chini mkateke maji. Tunachohitaji, usiku wa leo, ni maji ya Mungu. Hilo ono lilitafsiri kabisa mapenzi ya Mungu kwa hao watu wanaokufa, wanaoangamia. Ono, usiku wa leo, la Bwana kusafisha kitu hiki na kuanza upya: Safisha, si kuanzisha madhehebu mapya, kuanzisha uamsho katika dhehebu. Anzisha mkutano mpya, anzeni kumwacha Mungu aingie. Chimbueni maskini kutafuta-tafuta makosa kwenu kote, na kusengenyana, na shingo ngumu, na ushirikina huu wote, na kutokuamini, tupeni kitu hicho nje.

171 "Vema, nakwambia, lakini Ndugu Branham, li—lingemaanisha *hivi*." Sijali inamaanisha nini, ama utachimba au ufe. Ninyi nyote Wamethodisti wa Chicago, anzeni kuchimba; Wabaptisti wa Chicago, anzeni kuchimba la sivyo mtaangamia; Wapentekoste wa Chicago, anzeni kuchimba ama mwangamie, chimbueni vitu hivyo, vitupeni nje. Ninawaambia BWANA

ASEMA HIVI, msipochimbua na kuutoa uharibifu huu ulio humo ndani, mtaangamia, nalo tunda na kanisa lenu vitakauka na kufa. Chimbueni.

172 Hamtasikia mvua nyingine ya vuli, ama mvua nyingine ya masika, ama chochote kile, bali kutakuwa na maji na amani kama mto, yakibubujikia kupitia kila moyo. Naam, bwana. Mtaona ishara na maajabu, na miujiza, na nguvu za Mungu zikirudi Kanisani, katika Pentekoste halisi, inayobubujika, ikishuka tu. Naam, bwana.

173 Naam, bwana. Ujumbe wa Roho: Tutaanza kuchimba au kuanza kuangamia. Nao walikuwa tayari wanaangamia, kwa hiyo iliwabidi kuichimbua. Chimbueni, msafishwe, kilindi zaidi, kadiri mnavyozidi kuchimba, ndivyo mtakavyokuwa bora zaidi. Mifumo ya kikanisa imeziba mifereji yote, yavuteni hayo magogo ya kale mkayatoe: "Siku za miujiza zimepita. Hatuhitaji uponyaji wa Kiungu siku hizi." Mbona, tunauhitaji zaidi siku hizi kuliko tulivyowahi kuuhitaji.

Mnasema, "Tuna madaktari walio bora kuliko wote." Hiyo ni kweli. "Tunazo dawa zilizo bora zaidi." Sawa. "Tuna hospitali bora zaidi." Kweli.

Tuna magonjwa mengi zaidi. Kweli. Maana mna kutokuamini kwingi zaidi. Kweli. Hivyo ndivyo hasa. Watu hawaninii . . .

174 Sasa, mnaona yeye alisema, "Sasa . . . " Kesho yake asubuhi, walifanya nini? Ninaweza kuwazia hao Waebrania huko nje wakisema, "Nilisikia lile ono la Bwana, nabii alisema kweli, nitakichimbua kitu hiki." Akagonga gogo la kale pale, "Ni kitu gani hiki? Ati asilimia kumi ya mshahara wangu? Vema, tumekuwa na milo ya supu ya jioni kumlipa mhubiri wetu." Chimbua gogo hilo litoke hapo, litoe hapo, unawiwa na Mungu sehemu ya kumi. Lichimbue, ukalitupe upande mmoja.

175 Moja kwa moja, akagonga gogo lingine dogo, "Loo, ni kitu gani hicho?" "Vema sasa, usiingie wazimu." Kivute kitu hicho na kukitupa nje, hicho ndicho kilichokupotosha. Naam, bwana. Tupa nje kitu hicho. Kadiri unavyochimba kwa kilindi zaidi, ndivyo utakavyopata maji mengi zaidi. Endelea tu kuchimba katika ghala ya Mungu, huku ukitupa kitu hicho nje mpaka ufikie mahali ambapo unaweza kujawa na maji halisi ya Uzima.

176 Ndipo mnamo mapambazuko, ilitokea kwamba waliona, maji yalikuja wala hawakujua yalikotoka. Yalikuwapo wakati wote, waliyaziba tu. Kuna nguvu Kanisani. Ninaweza kuwaambia, na nitamwambia mhudumu yeyote, ninaweza kuwaonyesha mahali ambapo Mungu alilipa Kanisa nguvu za kuwaponya wagonjwa, kutoa pepo, na kufanya mambo haya yote. Na sasa njoo uweke kidole chako kwenye Maandiko ambapo Yesu alisema, "Sasa, ninaziondoa Kanisani sasa."

177 Vema basi, imekuwaje? Kuna nini? Mliziziba, wazo lenu la kujibunia limeziziba. Ninaweza kuwaambia mahali ambapo Yesu aliahidi katika siku hii ya mwisho, na kuwaonyesha ya kwamba ishara hizi mnazoziona zikifanywa, kwamba Roho wa Mungu angekuja Kanisani na kuonyesha maono, na kadhalika namna hiyo, kama anavyofanya, basi ja—jaribu kulikanusha wakati mmoja uone mahali ulipo.

178 Sababu mambo haya ni kwamba, nyote mmezibwa na mifumo mingi sana ya kikanisa ndani yenu, yote imezibwa. Chimbueni kitu hicho, na mkakitupilie mbali, na kuacha maji yatiririke.

179 Kwenye mapambazuko, loo, ndugu, maji yanatiririka kwa njia huru, yakitoka kwenye ule Mwamba uliopigwa ambao ungali ulikuwa huko nje nyikani. Ni yeye yule jana, leo, na hata milele, jambo pekee unalopaswa kufanya ni kuondolea mbali magogo yote ya kale.

180 Ondolea mbali maskini kutokuamini kwote, okota kutokuamini huko na ukutupilie mbali, useme, "Vema sasa, sikilizeni, Yesu aliahidi jambo hilo, nami sijali mtu yeyote anasema nini, ninaliamini." Jambo ndilo hilo. Chukua hilo gogo ulitupe nje, useme, "Mungu aliahidi hilo, ninaliona papa hapa mbele yangu, sikuzote nimelidhihaki, nilifikiri lilikuwa ni kosa, lakini sasa nitaliamini, kwa hiyo nitalichukua hili gogo kuukuu na kulitupa nje." Na mara utakapoliondolea mbali hilo gogo, maji matamu ya amani ya Mungu yataanza kutiririka, kama mto, yatatiririka kupitia kwako.

181 Unasema, "Vema, sikuzote ni—nilishangaa kuhusu uponyaji." Hili hapa ndilo ninalowapata watu, uponyaji: Mungu anapokuja hapa na kujithibitisha Mwenyewe kuwa papa hapa miongoni mwenu, mnajua ni nini? Unanyosha mkono, unajaribu kutia imani kwa okidi, imani ilipakwa kwa magugu, hisopo. Hisopo ni magugu ya kawaida tu.

182 Ukijaribu kuchochea imani, huwezi kuichochea imani. Imani ni ya kawaida sana, ni imani ile ile unayoenda kuchota maji ya kunywa nayo, imani ile ile unayo—unayoliendesha gari lako nayo. Unaona, ni ya kawaida tu. Wewe. . .Vema, hisopo, unaweza kuiona ikikua ardhini, kutoka kwenye nyufa za jengo, popote pale. Basi walipoipaka ile damu kwa hisopo, walikuwa wakipaka imani.

183 Unapaka imani kwa ninii ya kawai-. . .kupaka Damu kwa kitu cha kawaida tu, kama imani-magugu. Lakini unajaribu kuangalia kila mahali na kusema, "Laiti ningaliweza tu kupata okidi ya kupaka ninii yangu, yale ninayoamini katika Yesu! Laiti ningeweza tu kunyosha mkono na kushika okidi!" Huhitaji okidi, chukua magugu yaliyo papo hapo karibu nawe. Chukua imani unayoenda nayo nyumbani, chukua imani iliyokuleta hapa. Tumia kitu hicho hicho usiku wa leo, upate kuona

kitakachotukia, loo, ndugu, kamwe hakutakuwa na shaka niani mwako, kama kweli, Damu inapakwa na imani ya namna hiyo, sijali.

184 Unasema, "Yesu Kristo ni yeye yule jana na hata milele. Ninatupilia mbali magogo yote ya kale ya ukasisi na kila kitu, kutoka kwenye mfumo wangu, papa hapa sasa, na Bwana Mungu, kwa imani ya kawaida tu ambapo ninakuamini Wewe kuwa Mwokozi wangu, Wewe ni Mponyaji wangu." Amina. Amina. Amini hilo namna hiyo, na uhisi tu amani kama mto. Yale mabubujiko makubwa kutoka kwenye Chemchemi hiyo isiyokauka kamwe, Chemchemi hiyo itabubujika tu, utakapoondosha magogo yote ya kale, endelea tu kuchimba.

Kama ukigonga kitu humo ndani kinachokufanya. . . Kama umefanya kosa, sema, "Ni—ninadaiwa pesa na *Nanii*." Vema, nenda ukailipe.

185 Unasema, "Vema, siwezi kumlipa." Nenda ukamwambie kuihusu basi. Hiyo ni kweli. Usirefushe maneno kuihusu, nenda ukamwambie. Unaona? Kisha umwambie, useme, "Nitalisahihisha, Ndugu, nipe tu muda kidogo. Ninajiandaa kuliweka sawa."

"Vema, hebu nikwambie, niliwadhihaki hao watu walioitwa Wapentekoste."

186 Simama na kusema, "Ninasikitika nilifanya hivyo." Hiyo ni kweli. Sema, "Bwana, unaujua moyo wangu. Enyi watu, nisameheni." Nawe utasikia hilo gogo la kale likitoka, maji mengine yataanza kumiminika ndani, loo, jamani, yataendelea tu kuingia ndani.

187 Muda si muda wajua, useme, "Daima nilidhani hayo maono yalikuwa ya ibilisi, bali naona sasa ni ya Mungu." Vema, basi hilo gogo la kale litaondoka, ndipo maji yataanza kumiminika ndani tena. Hiyo ni kweli. Toa tu kila kitu hapo kwenye mtaro, maji yapo. Mnaamini?

188 Biblia ilisema, "Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele." Kwa hiyo Yeye angali ni ule Mwamba uliopigwa, Yeye angali ana Uzima, angali ana maji, ana nguvu za uponyaji. Unasema, "Ndugu Branham, je, Yesu ataniponya?" Tayari anao, ondoa tu hayo magogo njiani.

189 Ondoa takataka zote, na ndoo kuukuu, na mabirika, *phhh, hmm*! Ondoa vitu hivyo vyote njiani. Maskini farasi waliokufa, na mambo ya kikanisa yaliyoko njiani mwako, tupilia mbali kitu hicho, Mungu hataingia kwa ukani-. . . utayachafua hayo maji. Nayo hayo maji hayatachafuliwa, kwa hiyo ondoa tu uchafu wako mwenyewe, wa kutokuamini, ndipo Mungu atayamiminia maji ndani, tayari yapo, jambo pekee unalopaswa kufanya ni kuondoa tu chanzo chake, tiba tayari imefanywa.

190 Mungu tayari amekuponya, inakubidi tu kuondolea mbali kutokuamini kwako; hilo ndilo ono. Ninasema hilo katika Jina la Bwana, kama vile Elisha alivyosema siku ile, BWANA ASEMA HIVI, ondolea mbali kutokuamini kwako, angalia kitakachotukia.

191 Ondoeni mifumo yenu kwenye njia, angalieni ni uamsho gani utakaoipiga Chicago. Angalieni ni uamsho wa jinsi gani utakaoupiga ulimwengu, kama tukiondoa mifumo yetu kwenye njia. Tuondolee mbali mawazo yetu wenyewe na kuacha . . . Roho tayari . . . Mwamba tayari umepigwa, jambo pekee tunalopaswa kufanya, ondolea mbali tu hivyo vitu na kuyaacha yatiririke. Unataka kuona watu wakiponywa? Unataka kuponywa wewe mwenyewe? Ondolea mbali tu mashaka yote, kisha uone kitakachotukia, yatatiririka kama mto.

192 Ndipo kesho yake asubuhi, adui akaangalia juu, naye akaangalia upande wa pili pale, na alipofanya hivyo, ilikuwa ni maji, lakini kwa adui, jinsi jua lilivyokuwa likiwaka, ila tu lilionekana kama damu, nalo lilimtisha. Hiyo ni kweli. Ndipo likaingiza wazo dogo, la kipumbavu akilini mwake, likamnasa moja kwa moja ndani yake.

193 Nabii aliwaambia nini? Kasema, "Mbona, sasa, hili ni jambo dogo kwa Bwana. Kama nyote mkiondolea mbali hayo magogo yote, nitashughulikia yaliyosalia." Kama mtaondoa—kama mkiondolea mbali kutokuamini kwote, Mungu atashughulikia hayo mengine.

194 Mnajua kilichotukia? Alisema, "Kila mtu, okoteni jiwe. Nami nitawapa hiyo nchi, nitawaruhusu kuimiliki." Basi kila mtu akaokota jiwe na alipofika kule ambako maskini hivyo visima vya kawaida vilikuwa, alikuwa na ushuhuda mzuri wa jiwe. Amina. "Mungu asifiwe! Mungu nipe Roho Mtakatifu. Mimi ni—mimi ni kama Simoni, mimi ni Petro sasa, jiwe dogo." Amina. Ndipo kila mtu akashika jiwe lake mwenyewe mkononi mwake, ushuhuda halisi, la ushuhuda halisi, motomoto!

195 Wakati Yesu alipokuja mbele ya Petro, alisema, "Jina lako ni Simoni. Na tangu sasa, utaitwa Petro, ambalo ni 'jiwe dogo.'" Ndugu, alilichukua hilo, alijua Huyo alikuwa ndiye Masihi, huyo akaenda zake na kuziba visima vya kawaida kwalo.

196 Basi tunachohitaji usiku wa leo, ni kupata ushuhuda wa namna iyo hiyo, kujua ya kwamba Yesu Kristo yu hai na Yeye . . . Utakomesha shuhuda hizi zote za kawaida, zinazosema, "Siku za miujiza zimepita. Hakuna kitu kama hicho." Hayo mabirika ya kale yaliyovunjika, hata hivyo, vifurukuta mikia ndani yake, yatayaziba.

197 Hebu tupa jiwe hilo la ushuhuda huko nje, "Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele," ingia katika Roho, huna budi kuingia katika Roho.

198 Ukienda kwenye dansi na kuanza kucheza, wanaanza kupiga makofi yao, wakicheza dansi hiyo yote, unasimama huko, ukisema, "Hum, um-hum." Ninii yako yote . . . Hivi usingekuwa mcheza dansi? "Hakika. Naam." Hakika uko katika *roho* yake. La, wanaifurahia, na kucheza, na kupiga makelele, na kupiga mayowe.

199 Hivyo ndivyo unavyopata uamsho. Ni wakati kweli unapoingia katika Roho wa uamsho, si kuuchochea, ama chochote kile, bali kwa kuushusha kwa maombi, mpaka kuwe na uamsho unaoupiga moyo wako, mpaka magogo yote ya ukanisa, na magogo yote ya ulokole, na magogo yote ya mifumo, na magogo yote ya kutokuamini yanaondolewa, ndipo maji ya Mungu yanakububujikia. Haya basi.

200 Ndipo ushuhuda wako basi: Hutakuwa ukivuta sigara nyuma ya nyumba, na huku nje usiku wa leo, ukirukaruka kanisani, na kusema una Roho Mtakatifu. Wewe ni shaba iliayo na upatu uvumao, watu wanajua hilo. Unapotoka hapa nje pamoja na maisha haya yote ya namna hii, wanawake wakikata nywele zao, na kujipaka rangi midomoni mwao, na kusema, "Mimi ni Mpentekoste." Loo, ewe maskini, mwenye mashaka . . . ? . . .

201 Baadhi yenu wahubiri mlio na mashemasi kanisani mwenu, huku wakiwa na wake wanne ama watano mbalimbali na mambo kama hayo, wakisema, "Mimi ni Mpentekoste." Loo, loo, loo, loo, loo, loo, loo! Ulimwengu una akili bora kuliko hiyo, wao ni werevu kuliko hivyo. Naam, bwana. Loo, jamani!

202 Unatoka hapa nje, unaweka dau kwenye mashindano ya farasi na kadhalika, kisha unajiita mwenyewe, na wengi wenu mngekaa nyumbani na kusikiliza televisheni kabla ya kwenda kwenye mkutano wa maombi, na kusema, "Mimi ni Mpentekoste." Loo, loo! Umepewa tu *jina* la Mpentekoste, huna *tukio* la Kipentekoste. Kanisa ndilo kitu cha kwanza moyoni mwako, ndugu. Hilo ndilo yote katika yote, ni Mungu, Mungu, ndiye yote unayeweza kuona na kujua habari zake, ni Mungu.

203 Hilo ndilo kundi *linalojiita* Pentekoste, na kusema, "Aa, sasa kitu hicho ni upuuzi, usiamini hilo." Unaona? Lakini ono la Bwana huja kwa Neno la Bwana. Chimbueni hayo yote, chimbueni kutokuamini huko kwote kusudi maji ya Uzima yaweze kutiririka ndani kwa njia huru, na atakomesha haya yote hapa akisema, "Siku za miujiza zimepita." Hebu Kanisa lirudi kweli.

204 Unasema, "Wapentekoste si kitu ila kundi tu la kujisingizia imani." Shuka moja kwa moja na kuchimba chini mpaka ufikie kiwango cha chini kabisa, hebu upate tukio la Kipentekoste ndipo uone kitakachotukia, ndugu, hakuna mtu anayeweza kuyanyoshea kidole maisha yako. Naam, bwana. Wewe ni mraba kama, uh, mnyofu kama mtutu wa bunduki, nawe ni muungwana

kwelikweli, wewe ni mtu halisi wa Mungu, wewe ni mwanamke halisi wa Mungu.

205 Unapotiwa muhuri na Roho Mtakatifu, huo muhuri uko pande zote mbili za karatasi, wanaweza kukuona ukija, wakuone ukienda. Watajua ya kwamba unaonekana kama, unatenda kama, unaongea kama, na—na—na kushirikiana kama, nawe ni Mkristo, wakati umetiwa muhuri na Roho Mtakatifu. Wewe . . . Mungu yuko tayari kufanya jambo hilo, kama tuko tayari kumwacha afanye hivyo. Mnaamini hilo?

206 Sasa, jambo la pili la kufanya ni nini? "Jambo la pili, Mhubiri, ni wewe kuja kuniwekea mikono?" Hilo halina uhusiano wowote nalo, hilo huenda likakufanya, likakuchochea kwemye kitu fulani kidogo, bali hilo—hilo silo. Jambo la kufanya, ndugu, ni kukubali Neno la Mungu na kusema, "Ni kweli nami ninaliamini. Nami nimepata vipande vya kale humu ndani, ninatupa nje sasa hivi, kutokuamini kwangu, nami ninalitatua na Mungu, Nitaamini." Amini kwa ajili ya wokovu wako.

207 Sasa, sasa, siwezi kukwambia kuhusu wokovu wako, inakubidi kuushughulikia huo mwenyewe. Lakini Kristo angali hai na anatawala. Yuko hapa usiku wa leo. Unaamini hilo? Una nini, cha kufanya? Ingia katika Roho, ndipo unapoingia katika Roho, basi unaona ono.

208 Lakini maadamu unasema, "Vema, Mungu abarikiwe, mimi ni Mmethodisti. Sio lazima nivumilie mambo kama hayo." "Mimi ni Mbaptisti." "Mimi ni Assemblies." "Mimi ni wa Umoja." Vema, endelea, kamwe hutaona hilo ono. Lakini wewe tupa kitu hicho kando na uingie kwenye ono, umwone Yesu akija huku kanisa likiangamia hapa, kisha uingie katika ono, chimba chini kabisa, ndugu, nakwambia, jambo fulani litakupata basi, utaingia katika Roho ya uamsho. Unaamini hilo?

Hebu sote na tuingie katika Roho basi na kuliamini. Na tuinamishe vichwa vyetu tunapomwomba atupe maono.

209 Baba wa Mbinguni, tuko katika nchi inayoangamia, tuko katika taifa linaloangamia, tuko katika ulimwengu unaoangamia, na kuwahubiria watu wanaoangamia. Nami ni, mimi ni mwanadamu tu, na hawa wahubiri wengine ni wanadamu tu, bali Wewe ni Mungu asiyeharibika.

210 Ninakuomba Wewe usiku wa leo, Bwana, ya kwamba ujumbe huu ambao nimeunena, na miezi yangu sita ya wasiwasi ya kwenda na kumalizia, huenda sikuusema vizuri kabisa, Bwana, lakini kama mimi—kama sikuusema vizuri, Wewe mwache Roho Mtakatifu aulainishe na kuondoa makunyanzi yote, Mungu, kama tu vile ulivyomfanyia Ibrahimu. Naye akasema, tunajua alikuwa na mahangaiko yake, naye—naye akayumbayumba, na, lakini wakati maelezo ya Kiungu ya maisha yake yalipoandikwa, mbona, yalisema hakusita katika

ahadi ya Mungu kwa kutokuamini, bali alikuwa na nguvu, akimsifu Mungu.

211 Kwa hiyo Bwana Mungu, maskini kusitasita kwangu kwote, na maneno yaliyoendelezwa vibaya, na kutamkwa vibaya, na kadhalika, jalia Roho Mtakatifu ayalainishe tu, na kuweka maelezo halisi ya Kiungu katika kila moyo wa ujumbe huu usiku wa leo, tunaoishi.

212 Na bado kungali na mtumishi wa Mungu, bado kungali kuna watu wanaompenda Mungu, na kuna Mungu Ambaye anawajali, na kuna Mwokozi aliyepigwa miaka elfu mbili iliyopita, aliyejeruhiwa kwa makosa yetu, akachubuliwa kwa maovu yetu, adhabu ya amani yetu ilikuwa juu Yake na kwa kupigwa Kwake sisi *tuliponywa*, Mwokozi yeye yule aliyesema, "Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya."

213 Mungu, jalia kila fungu la kale liondolewe, na kila ndoo ya kale yenye kutu, na kadhalika viondolewe njiani usiku wa leo, na jalia maji ya Uzima yatiririke kwa njia huru. Mungu nipindue ndani nje na kuniosha na kunitakasa, Bwana, na unijaze na Roho Wako sasa hivi. Na uwajaze watu hawa hapa nje kwa imani, ili kwamba kukiwako na mmoja hapa chini ambaye haamini, wapate kuona na kuamini, kwa sababu tunaomba, katika Jina la Yesu. Na jalia ninii. . .ndipo wao, kila mmoja, aingie katika Roho nasi sote tujazwe na Roho, na wote waponywe na kuokolewa usiku wa leo. Kwa kuwa tunaomba, katika Jina la Yesu. Amina.

> Kuna Chemchemi iliyojaa Damu,
> Iliyotolewa kwenye mishipa ya Imanueli,
> Na wenye dhambi wakitumbukizwa chini ya gharika hiyo,
> Hupoteza madoa yao yote ya hatia.
> Hupoteza madoa yao yote ya hatia,

Hebu tuinue tu mikono yetu, huku. . .

> . . .madoa yao yote ya hatia;
> Na wenye dhambi wakitumbukizwa chini ya gharika hiyo,
> Hupoteza madoa yao yote ya hatia.

Na tuinamishe vichwa vyetu sasa.

> Aliyekuwa akifa. . .[Ndugu Branham anavumisha—Mh.]

214 Ee Baba Mungu, tunakufa sasa kwa kutokuamini kwetu kwote. Umba ndani yetu sha—shauku ya kuchimba sasa. Tunachimba, Baba. Nichunguze na unijaribu uone kama kuna kutokuamini ndani yangu, Bwana, kukiwapo, nisaidie kukuondolea mbali sasa hivi. Nisaidie kuusafisha huu, mfereji, kusudi nguvu za Mungu ziweze kupitia.

215 Lisaidie kusanyiko hili sasa hivi, Bwana, ninawaombea. Ninaomba ya kwamba utajalia kila mfereji uwe safi. Safisha kila kanisa lililowakilishwa hapa, Bwana, yote, kutoka dhehebu moja hadi lingine, safisha kabisa na kuondoa kutokuamini kwote, Bwana. Safisha na kuondolea mifumo yote ya ulimwengu kutoka kwake, jalia ushirika mtamu wa Roho Mtakatifu uingie kupitia mifereji ya Mungu, ukipitia hapa usiku wa leo, akileta ufunuo mpya, Neno la Uzima, jalia litoke usiku wa leo, liingie katika kila nafsi hapa.

216 Nami ninajua Wewe upo hapa, Bwana. Nao wananiangalia kama mwonaji Wako, kama mwaminio Wako, kama mtu wa kufanya mfano. Na Baba Mungu, ninaomba ya kwamba utanisaidia usiku wa leo, kusudi Roho Mtakatifu apate kiingilio huru ndani ya nafsi yangu, na moyoni mwangu, maisha yangu, macho yangu, utu wangu, si kwangu tu bali kwa kila mtu hapa, ili wale wasioamini, wapate kumwona Roho akitenda kazi kupitia kwa waaminio na kusema, "Kama, hayo maji yanaweza kutiririka kutoka kwenye Mwamba huo uliopigwa kupitia kwao, yanaweza kupitia kwangu, pia." Tujalie, Baba. Ninaomba, katika Jina la Yesu. Amina.

217 Pia Baba, ninaomba ya kwamba utawabariki ndugu zangu hapa, nyuma yangu, watu hawa wa thamani, baadhi yao walikuwa wakihubiri Injili nilipokuwa mvulana mwenye dhambi, Mungu, tujalie usiku wa leo, baadhi ya watu hawa wanaoketi hapa, wamekuwa hudumani kwa muda mrefu, wao ni mashujaa, wana makovu.

218 Mara nyingi mifumo huwaongoza watu, wakati mwingine, kuninii. . .lakini ndani ya moyo wao Bwana, wao—wao—wao wanataka kuona matendo ya Mungu. Ndipo tunaona ya kwamba ibilisi asipofanya jambo *moja*, atafanya *lingine*, na halafu atavuruga kitu fulani, ama kuchafua kitu fulani, nacho kwa namna fulani kinawafanya warudi nyuma kidogo. Baba, jalia kila moyo ufunguliwe, usiku wa leo, kwenye Chemchemi halisi.

219 Sasa, Mungu, ninaweza kunena, mimi ni mwanadamu tu, ningeweza, huenda nikatoa tamshi la namna yoyote, huenda nikalifanya lisikike sawa, lakini hata hivyo isingekuwa ni Wewe, Neno moja tu kutoka Kwako litathibitisha jambo hilo, Bwana. Ulisema, "Akiwepo mmoja miongoni mwenu aliye na—nabii ama wa kiroho, Mimi Bwana nitasema naye, nitamwonyesha maono, ninene naye katika ndoto. Na kama yale asemayo yakitimia, basi msikieni, lakini yasipotimia, msimwogope mtu huyo, kwa sababu siko pamoja naye, lakini likitimia, basi lisikieni."

220 Sasa, Baba Mungu, nilithibitisha hilo, ama, usiku wa leo kwa Maandiko na kila usiku, ya kwamba Wewe ni Kristo, Wewe ni—Wewe ni Mwana wa Mungu. Nawe ulipigwa upate kuondoa dhambi zetu na kutokuamini, ili Uzima Wako Mwenyewe utiririke kupitia kwetu. Sasa ninawaambia watu ya kwamba

Wewe umeketi mkono wa kuume wa Mungu usiku wa leo, huko Juu, huko juu kwenye Kiti cha Enzi, Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu. Tujalie, Bwana, ya kwamba kutakuwa na matatizo mengi ya damu usiku wa leo, yatakayokomeshwa, kwa sababu ya kusambaa kwa kutokuamini. Kwa kuwa ninaomba hilo, katika Jina la Kristo. Amina.

221 Siamini tumekuwa na kadi ya maombi tangu Jumapili iliyopita alasiri, vizuri sana ninavyokumbuka, hatujaitisha mstari wa maombi. Lakini kila usiku, Roho Mtakatifu ametoka akaenda moja kwa moja miongoni mwa watu. Ni wangapi wanaojua hilo kuwa ni kweli? Kumi, kumi na tano, na kadhalika, kila usiku, kote huko nje, watu msio na kadi zenu za maombi.

222 Kwa namna fulani ninajisikia mwenye hatia kwa kutochukua baadhi ya hizo kadi. Nami najua nimechelewa kidogo tu, lakini nilisema jana usiku, nilikuwa nimechelewa tena, nikasema, "Kesho usiku tutajaribu kugawa kadi za maombi." Naye Billy, nilimtuma usiku wa leo, na kumwambia, "Gawa baadhi ya kadi za maombi." Kwa hiyo akazigawa.

223 Aliniambia alitoa B, moja hadi hamsini? Moja hadi mia moja? B, moja hadi mia moja. Vema. Walianzia mahali hapo. Tulikuwa wapi, tulianza ule wakati mwingine, tulianzia kutoka moja ule wakati mwingine, sivyo? Loo, naam, tulikuwa na siku mbili usiku, samahani. Ule wakati mwingine tulianzia kwenye B, tulianzia themanini, moja hadi—moja hadi ishirini na tano, kisha tukaanzia themanini na tano hadi mia moja.

Vema, hebu na tuanzie katikati basi, usiku wa leo. Hebu tuanzie ishirini na tano hadi—ishirini na tano hadi hamsini, tuseme. Hilo litakuwaje?

224 Ni nani aliye na B, ishirini na tano? Inua mkono wako. Mwanamke fulani pale? Njoo moja kwa moja hapa, mama. Ishirini na tano, ishirini na sita? Vema, mama, njoo huku juu. Wako kote jengoni.

225 Sasa, mvulana huyo anapokuja kutoa kadi hizi, yeye huja na kuzichanganya mbele zenu, ili kwamba akupe tu kadi, popote ilipo, nasi tunawaita kuanzia mahali fulani. Mnaona, ninii, hakuna mtu ajuaye mahali hizi zitakapoanzia, tunaanzia tu mahali pamoja hadi pengine.

226 Sasa, ni wapi. . .? Ishirini na tano, sivyo? Ishirini na sita? Ishirini na tano, ishirini na sita, ni nani aliye na ishirini na sita? Vema, ishirini na sita, papa hapa. Ishirini na saba. Ni nani aliye na kadi ya maombi namba B, ishirini na saba? B kama katika—katika Boston, ishirini na saba. Vema, ishirini na nane, ni nani aliye na ishirini na nane? Siuoni huo mkono, tafadhali. Ishirini na tisa? Thelathini? Thelathini na moja, ni nani aliye na thelathini na moja?

227 Laiti ungengojea tu mpaka niite namba yako ili nipate kuwa na uhakika. Kwa sababu mtu fulani ni kiziwi, ama chochote kile, wanasema, "Ndugu Branham," wananiandikia kadi, "na—namba yangu iliitwa, lakini nilikuwa kiziwi wala hakuna mtu aliyeniambia nawe u—ukadhani, walisema ulidhani nimetoka nje." Na huenda-. . . "Ni—nilikuwa kiwete, hata nisingeweza kuinua mkono wangu, wa—wala hakuna aliyeniinua." Mnaona? "Na hata sikuombewa."

228 Unaombewa, kipenzi-mtoto, unaombewa kila usiku. Yesu, sasa hivi, anakuombea, kwenye mkono wa kuume wa Ukuu, Naye anakutaka tu umwamini.

229 Vema. Nilikuwa wapi? Ishirini na sita? Ishirini na moja, -mbili? Vipi. . .? Wapi—wapi, Ndugu? Thelathini na moja. Thelathini na mbili, thelathini na mbili. Vema. Thelathini na tatu. Thelathini na nne. Thelathini na nne. Siioni, thelathini—thelathini na nne. Kadi ya maombi namba thelathini na nne. Ukipata kadi. . .Mtu fulani aangalie kote, labda mtu fulani ni kiziwi, bubu, ama hawezi kusimama. Thelathini na nne, sitaki kuikosa. Labda walitoka nje. Thelathini na nne, thelathini na tano. B, thelathini na tano. Vema. Vema. Thelathini na nne, thelathini na nne ameingia kufikia sasa? Thelathini na nne, B, thelathini na nne. Thelathini na tano alikuwa mle ndani. Thelathini na sita.

230 Usiogope. Kama ukitenda dhambi, iungame, na, ukifanya vibaya, basi ingefunikwa na Damu utakapofika hapa. Unajua kinachotukia unapofika hapa kama una dhambi isiyoungamwa, sivyo? Vema, usichukue kadi basi. Omba kabisa kwanza, ndipo uchukue kadi. Unaona?

231 Vema, hebu tuanzishe mstari wa maombi, basi. Vema. Sijui, mna wangapi hapo? Moja, mbili, tatu, nne, tano, sita, saba, nane. Tatu ni shahidi. Hilo litakuwa zuri vya kutosha. Vema.

232 Vipi ninyi huko nje msio na kadi ya maombi? Hebu tukuone ukiinua mkono wako. Wewe ni mgonjwa na unataka Mungu akuponye. Popote humu jengoni, sijali uko wapi. Ati nini? Thelathini na sita, thelathini na saba, thelathini na nane, thelathini na tisa, arobaini. Wanakuja wawili kutoka kwa hiyo. Arobaini hadi hamsini. Watatu. Mwingine. (Nafikiri ninakosea, sivyo? Ninapaswa kuhubiri tu na kuita wito wa madhabahuni.) Vema. Sawa, hebu tuanzishe mstari wa maombi sasa, tafadhalini.

233 Kila mtu awe na kicho kabisa, kila mtu awe na kicho tu uwezavyo kuwa sasa. Na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo tu. *Amini Tu*, Ndugu, tafadhali.

Ninii tu. . .

Umekuwa ujumbe mgumu sana, usiku wa leo. Tunataka Roho aje sasa.

. . . amini tu,

234 Sasa, wakati wanapokuja, ningetaka kuuliza hivi: Kama—kama Kristo anaweza kujithibitisha Mwenyewe kuwa hapa, ni wangapi wenu watakaomwamini kwa moyo wenu wote, utatupa kila kipande nje? Je, kuna mtu yeyote ambaye hajawahi kuwa katika mmoja wa mikutano yangu hapo kabla? Inua mkono wako. Hujawahi kuwa katika mmoja wa mikutano yangu. Ni jambo jema kwamba wote hawaji usiku ule ule.

235 Vema ndugu, nyote niombeeni, sivyo? . . . ? . . . [Ndugu Branham anazungumza na ndugu jukwaani, mengi ya maneno yake hayatambuliki. Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

236 Ndugu zangu, nilikuwa tu nikiwauliza, kundi hili nyuma yangu, nitaliweka kundi hilo huko nyuma likiomba, jambo fulani halina budi kutukia, watu halisi wa Mungu.

237 Sasa iweni tu na imani. Vema, nadhani mandhari ingeanza usiku wa leo . . . Ni—ninataka kuwaambia kwanza ninyi watu, kila usiku kumekuwa na wengi sana, angalau siamini tumekuwa na usiku mmoja, isipokuwa tumekuwa na angalau visa maalum vinane, ama kumi, ama kumi na vitano kote jengoni. Hiyo ni kweli? Ninyi watu wote ambao mmekuwa hapa? Mnaona?

238 Sasa, kwenu ninyi wageni, sasa, sidai kuwa mponyaji wa Kiungu, siamini kuna mtu kama huyo duniani, ninaamini ya kwamba Yesu Kristo ndiye Mponyaji. Na Yeye—Yeye tayari amekufanyia kila kitu ambacho angeweza kufanya, kwa sababu wakati alipopigwa huko nyuma, Yeye alikuwa ndiye ule Mwamba. Mnaamini hilo? Yeye alikuwa Nguzo ya Moto, yule MIMI NIKO. Naye . . . Jambo pekee tunalopaswa kufanya ni kung'oa tu vizibo njiani. Hivi hamwamini hilo? Vema basi, Yeye tayari amemponya kila mgonjwa hapa, kila mtu tayari ameponywa, kila mwenye dhambi tayari ameokoka, lakini, ndugu, afadhali ulikubali, na, kwa ajili ya uponyaji wako.

239 Angalieni tu hapa, tulikuwa na mwanamke hapa hivi majuzi usiku, akitoa ushuhuda. Vema, walimleta kule maskanini, si muda mrefu uliopita, naye mwanamke huyo alikuwa mahututi kabisa namna *hii*, hata asingeweza kutembea, akiwa na uvimbe. Ilibidi wanaume wambebe na kumweka kwenye vipandio. Sikuwa nikiwaombea wagonjwa usiku huo, naye akanishika kwa mguu wa suruali, naamini ndivyo ilivyokuwa, nikitoka nje, ndipo nikageuka nikiwa na BWANA ASEMA HIVI.

240 Naye mwanamke huyo alikuwa hapa hivi majuzi usiku, akiwa mwembamba tu na wa kawaida awezavyo kuwa. Mnaona? Na wote . . . Loo, jamani! Hatujaribu . . . Si—siutangazi, na kadhalika, na kuendelea namna hiyo. Kwa sababu, mara nyingi, Yesu alisema . . .

241 Nafikiri shida ya siku hizi, tunaufanya uponyaji wa Kiungu kuwa kivutio kikubwa kupindukia. Mnaona? Si madoido. Hiyo ndiyo sababu nimewaambia, nami ninaamini

kwa moyo wangu wote, Chicago wanaliona hili kwa mara yao ya mwisho. Mnaona? Ninaamini hilo. Ninaamini wengine nchini, pia. Ninaondoka, mnaona, kwa hiyo ni—ninaamini. Nanyi mnakumbuka, mnakumbuka yale Yeye aliyosema, Yeye aliniambia yale niliyowaambia.

242 Sijawahi kuwaambia lolote katika Jina la Bwana, pasipo kutukia jinsi tu lilivyosemwa. Ninawaulizeni hilo sasa. Mnaona? Vema basi, niamininі. Kristo tayari amewaponya, hamna budi kulikubali. Lakini sasa, vipi kama Yeye alikuwa amesimama hapa na suti hii aliyonipa, amevaa suti hii? Sasa, kama ungemjia, useme, "Bwana, utaniponya?"

243 Angesema, "Yaondolee mbali magogo kutoka kwenye njia. Ninajaribu kusukuma nipate kuja kwenu, bali kutokuamini kwenu ndiko kunakowazuia."

244 Sasa, hapa—hapa ni, kwenu ninyi wageni, hii hapa ma—mandhari ya Biblia, Yesu katika ninii wa sa-. . . mlango wa 4 wa Yohana Mtakatifu, alimjia mwanamke kisimani, aliyeitwa. . . mwanamke Msamaria. Sisi sote tunaifahamu hadithi hiyo. Naye alijitambulishaje kwake kama Masihi? Yeye alifanya nini? Alisema. . . mwanamke huyo akamwambia, kasema. . . Akamwambia mwanamke huyo, "Nipe maji ninywe." Alikuwa akiwasiliana na roho yake.

245 Akasema, "Maji. . . kisima ni kirefu na huna kitu cha kuchotea." Naye akasema. . . Wao, vema, wakaanza kuzungumza juu ya dini basi, alitaka kuzungumza juu ya dini, "Sisi tunaabudu katika mlima huu, Wewe unasema huko Yerusalemu, maana. . . " Kasema, "Ha—hatupaswi kuwa tukishirikiana pamoja, kwa sababu Wewe ni Myahudi nami ni M—Msamaria."

Naye akasema, "Mwanamke, nenda kamwite mumeo, mje naye hapa."

Akasema, "Sina mume yeyote."

Kasema, "Umesema kweli. Umekuwa na watano, na yule unayeishi naye sasa siye mume wako."

246 Sasa, ile huduma ilisema nini juu ya jambo hilo katika siku hizo? Sasa, ninaposema *huduma*, sizungumzii wahudumu wa aina *hii*, hao ni ndugu, moyo kwa moyo pamoja nami. Ninamaanisha huduma inayodhihaki jambo hili, na kusema ni bure, si madhehebu yanayoniunga mkono, hao wanao, walio na mfumo wa Mungu ndani yao. Lakini ni hawa ambao hawaninii. . . wanaokana jambo hili, ndio ninaozungumzia, mnaona, kule kulikana, yule anayesema, "Ni bure, ni la ibilisi." Hivyo ndivyo walivyofanya huko nyuma.

247 Lakini maskini mwanamke huyo kahaba, alisema, "Bwana, naona kwamba Wewe ni Nabii. Sasa, tunajua, tumefundishwa, tunajua ya kwamba Masihi ajapo, Yeye atatwambia mambo haya." Sasa, ni wangapi wanajua hiyo ni kweli? Hiyo ni kweli.

Akasema, “Mimi ninayesema nawe Ndiye.”

248 Ndipo akakimbia mjini na kusema, “Njoni,” akawaambia—akawaambia hao watu, kasema, “njoni, mwone Mtu Ambaye ameniambia mambo ambayo—ambayo nimefanya. Haimkini Huyo kuwa ndiye Masihi?” Nayo Biblia ilisema mji mzima ukamwamini Yesu, Yeye hakufanya hivyo tena, alifanya hivyo wakati mmoja tu, kwa sababu mwanamke, mwanamke huyo kahaba, aliwaambia ya kwamba Yesu alimwambia ya kwamba alikuwa akiishi na mwanamume asiyefaa. Ndipo mji mzima ukaamini ya kwamba Yeye alikuwa ndiye Masihi, kwa sababu hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya Masihi.

249 Sasa, kama unafikiri ya kwamba theolojia ndiyo ishara ya Masihi, na—na hiyo ni—na hiyo ni ishara kuu kuliko *hii*, Yesu alisema, “Kazi nizifanyazo Mimi, ninyi nanyi mtazifanya,” nawe unasema kuhubiri Injili ndiyo kazi kubwa zaidi, vema, basi njoo hapa ukafanye hizo kazi ndogo zaidi. Hili hapa jukwaa, karibu. Panda hapa juu, upitie kwenye mstari huu wa maombi, acha Roho Mtakatifu atende kazi kwenye kusanyiko pale, juu yako. Hebu nikuone ukifanya kazi *hizo* na *ndipo* uende ukaihubiri Injili; ndipo ufanye, ufanye kazi kubwa zaidi.

250 Yesu asingeweza kuhubiri ubatizo wa Roho Mtakatifu, maana Huyo alikuwa hajaja bado. Hizo ndizo kazi kuu zaidi, na bila shaka ndizo. Kanisa linapaswa kuhubiri ubatizo wa Roho Mtakatifu, Yesu alisema unakuja, lakini Kanisa linao, likisema, “Tunao, na ni kwa ajili yako.” Mnaona? Kwa hiyo hizo zilikuwa *kubwa zaidi*, hiyo ni kweli. Lakini kazi *zile zile* alizofanya, “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya.”

251 Sasa, huyu hapa mwanamke ambaye simjui. Hatufahamiani. Sasa, kusudi kusanyiko liweze kuelewa. Sasa, mwangalieni huyu mama. Sikujui wewe, hatufahamiani, hii ndiyo mara yetu ya kwanza kukutana. Kama ndivyo ilivyo, inua mkono wako.

252 Sasa, hapa mwanamume na mwanamke wanakutana tena. Sina fununu zaidi ni gani, mwanamke huyo ni nani, ama kilichomleta hapa, ama, hata kidogo, hatufahamiani kabisa.

253 Sasa, huenda nikasimama hapa na kusema, kama, tuna saikolojia nyingi, nikisema, “Bwana ananiambia mtu fulani ana ugonjwa wa mgongo.” Hakika, wengi wao huko nje wana ugonjwa wa mgongo. “Wana shida ya mishipa.” Hakika, kundi kubwa lao. Mnaona?

Huyo ni nani? Yuko wapi? Alitoka wapi? Ni kitu gani kilichousababisha? Itakuwaje kwake? Hilo ndilo jambo linalofuata, mnaona, hilo ni tofauti.

254 Kama ningemleta mwanamke huyu hapa, niseme, “Bwana alinituma kuwaombea wagonjwa. Hebu nikuwekee mikono, nikupake mafuta. Utukufu kwa Mungu, utapona,” ana haki ya kuamini hilo, hiyo ni kweli. Lakini angeweza kulitilia shaka, juu ya ujuzi wangu, kama ninamwambia ukweli au

la, huenda akashuku hilo. Lakini wakati Roho Mtakatifu anapokuja na kunena kupitia midomo yangu na kumwambia jambo fulani ambalo *amekuwa*, hilo huondoa dosari kwake papo hapo. Mnaona? Maana anajua simjui. Nasi sote wawili tulimwinulia Mungu mikono yetu, hatufahamiani. Sasa, hiyo hapo Injili. Kama hiyo siyo Injili aliyokuwa nayo Kristo, kama hiyo haikuwa . . .

255 Unasema, "Ndugu Branham, unasema wewe ni Masihi?" Sasa, kama unawazia hilo, inaonyesha huna upambanuzi wowote wa kiroho. Unaona? Ningewezaje kuwa Masihi? Mimi ni William Branham, mwenye dhambi aliyeokolewa kwa neema, Yesu Kristo ndiye Masihi, bali Roho Wake yu hai ndani yetu, Roho Mtakatifu.

256 Na baadhi yenu ninyi watu ambao hamngeamini jambo hilo, Kitu hiki kinachowafanya watu hawa kulia, na kupaza sauti, na kunena kwa lugha, Roho yuyo huyo, Bi-. . .Paulo alisema, "Mtu akija miongoni mwenu, huku nyote mnanena kwa lugha, watasema mna kichaa, bali hebu mtu mmoja awe nabii na kuzifunua siri za moyo, ndipo wataanguka chini wakisema, 'Mungu yu pamoja nanyi,'" vema, mnaona, Hiyo—Hiyo ni Karama ya Kipentekoste, ndugu, Hiyo ni, Hiyo ni—Hiyo ni ninii tu, Hiyo ni—Hiyo ni Kitu fulani tu kilichoongezwa kwa Kanisa. Jinsi Wabaptisti na Wamethodisti walivyowapiga vita ninyi ndugu juu ya kunena kwa lugha, wananifanyia jambo lile lile juu ya jambo hili, kwa hiyo, bali itetee ile kweli. Mungu hana budi kuliachilia liendelee.

257 Iwapo sikujui wewe naye Bwana ataniambia kilichokuleta hapo, jambo fulani ambalo umefanya, jambo fulani unalopaswa kufanya, ama jambo fulani, dhambi fulani iliyo maishani mwako, ama—ama baraka fulani iliyo humo ndani, *kitu fulani* unachojua kama ni kweli ama si kweli, utajua kama hiyo ni kweli ama si kweli. Je, utaamini kwa moyo wako wote basi, ya kwamba ingekuwa . . .? Haina budi kuwa ni namna fulani ya nguvu za kiroho, maana hatufahamiani. Je, ungeamini ya kwamba ilikuwa—ilikuwa ni Masihi, sio mimi, bali ni Roho Wake akinena kupitia kwangu kama alivyoahidi?

Je, kanisa lote lingeamini hilo kwa moyo mmoja? Inua mkono wako. Asanteni. Sasa, wewe amini.

258 Mwanamke huyu amesimama kama futi kumi, kumi na mbili kutoka kwangu. Ninamwangalia tu kuzungumza naye, maana baada ya kuhubiri, na kadhalika, kama yule nabii alivyofanya kule chini, wala mimi si nabii, lakini kama vile nabii alivyofanya kule chini, yeye—yeye alikuwa akimkemea huyo Yehoramu pamoja na hao wengine, kwa hiyo ilimbidi tu kucheza na—na kuzungumza. Naye Yesu alizungumza na yule mwanamke, lakini kwanza ilimbidi kuwasiliana na roho yake mpaka alipopata upako.

259 Hilo ndilo ninalongojea sasa, kwa ajili ya, kuliondoa gogo la *William Branham* njiani, akili zangu, roho yangu, maari-. . . *kujua*, chochote kile, nami ninaondolea mbali hayo yote, kusudi aweze kutumia macho yangu, midomo yangu kujitukuza Mwenyewe mbele ya watu Wake, ku—kujisalimisha tu.

260 Kama hii *hapa*, kitu hicho hakiwezi kuzungumza hata kidogo, ni bubu. Lazima kuwe na kitu kilicho hai hapa, kikinena ndani yake kukifanya kinene, chenyewe hakiwezi kunena. Wala nisingeweza kukwambia lolote kukuhusu wewe, inahitaji Kitu fulani kilicho na Uzima wa Milele, Kitu fulani kinachokujua kuzungumza juu yake, hiyo ni kweli. Unaamini hilo.

261 Jambo moja ni matatizo yako, ni, kama watu wangali wanaweza kuisikia sauti yangu, ninaweza kumwona mwanamke huyo, ana wasiwasi sana na amefadhaika, anaugua ugonjwa wa wasiwasi. Sasa, hiyo ni kweli, kweli kabisa.

262 Sijui ni kwa nini, lakini kila wakati ninaposema tu jambo moja, kama nilivyosema daima, watu daima husema (nalihisi.), "Kubahatisha." Sibahatishi. Mnajua sikuwa na njia ya kubahatisha hilo.

Sasa, hiyo ilikuwa ni kweli? Kama hiyo ilikuwa ni kweli, yale yaliyosemwa . . .

263 Sasa, ni wangapi wanaoamini? Asanteni! Sasa, kama wewe. . .Kama vile Filipo, wakati alipomwambia mahali alipokuwa, jambo fulani kumhusu, alisema, "Rabi, Wewe ni Mwana wa Mungu, Mfalme wa Israeli."

Kasema, "Kwa sababu unaamini hilo, utaona makubwa zaidi." Hiyo ni kweli? Hiyo ni ahadi ile ile.

264 Simama mahali ulipo, sijui yale niliyokwambia yalikuwa ndio shida, lakini chochote kile, ulikuwa ni ugonjwa sahihi uliokuwa nao. Nini . . .? Naam, ninauona sasa, naam. Wasiwasi, umekuwa hivyo kwa muda mrefu sana, ulianza na wakati huu wa kukoma hedhi. Isitoshe, una matatizo ya kike, ni, ambayo yanakusumbua. Hiyo ni kweli.

265 Halafu jambo lingine, una mtu fulani moyoni mwako unayemwombea, hiyo ni kweli, sio hapa, shida ya macho, mama. Hiyo ni kweli. Sasa, unaamini? Mtumie leso hiyo ambayo wewe. . .wakati Roho Mtakatifu akiwa juu yako, kila kitu kitakuwa sawa. Nenda nyumbani. Mungu akubariki. Mungu akubariki, Dada.

Sasa, unaamini kwa moyo wako wote? Huna budi kuwa na imani, mtumaini tu Mungu. Sasa, umeshawishika ya kwamba Yesu Kristo . . .?

266 Sasa, msininii, tafadhalini msisogeesogee. Najua saa zinaenda. Hamtambui! Mnaona? Malaika wa Bwana alisema nini? "Ukiwafanya watu wakuamini." Halafu basi wakati wewe, ninaposema, "Kaeni kimya," nanyi hamfanyi hivyo, inafanya

nini? Inalitupa moja kwa moja usoni mwangu, Shetani anasema, "Unaona, hawakuamini." Baadhi yenu mnaniamini na wengine hamniamini, bali mnawaumiza wengine. Yesu aliwatoa wote ndani ya nyumba wakati mmoja.

267 Mnaona, ninajaribu kuwa mwinjilisti na mwonaji pia, wala huwezi kufanya hivyo. Ama nitaenda mwituni niwe mwonaji ndipo niingie kwa kishindo pamoja na ujumbe wangu na kurudi huko tena, au labda niuweke kando, naye Mungu auondoe kwangu, na kunijalia nihubiri Injili, na kuwa mwinjilisti.

268 U hali gani, Dada? Sikujui. Hatufahamiani. Hiyo ni kweli? Hatufahamiani. Ili kwamba watu wajue ya kwamba hatufahamiani, naomba uinue tu mkono wako, ya kwamba hatufahamiani. Kama Roho Mtakatifu atanifunulia kwa nini umesimama hapo, utaniamini mimi kuwa ni nabii Wake? Loo.

269 Huyu mwanamke anaonekana kuwa na roho nzuri, roho ya kuamini. Naam, bwana. Hii hapa inakuja. Anaugua ugonjwa wa moyo, ana ugonjwa wa moyo. Um-hum. Pia una yabisi kavu. Um-hum. Una ugonjwa wa wasiwasi. Una mtu fulani moyoni mwako unayemwombea. Kama Mungu ataniambia mtu huyo ni nani, ama kitu fulani kuwahusu, utaniamini mimi kuwa ni nabii Wake? Ni mtoto wako, binti, naye hayuko hapa, anaishi mbali sana na hapa, yuko California, naye anaugua ugonjwa wa fadhaa, BWANA ASEMA HIVI.

Sasa, unaamini kwa moyo wako wote? Basi nenda ukapokee. Kama tu vile umeomba na kuamini, ndivyo itakavyokuwa kwako. Vema.

270 Njoo, bwana. Sikujui wewe. Wakati mmoja Bwana wetu. . . Ninaamini hao wawili ama watatu wa mwisho waliopitia hapa wamekuwa—wamekuwa wanawake, na huyu ni mwanamume. Nilisema yale Yesu aliyomfanyia mwa—mwanamke, wakati alipokutana na mwanamke, sasa hebu nichukue mahali fulani katika Maandiko ambapo Yeye alikutana na mwanamume, kusudi wanawake na wanaume waweze kuona ya kwamba hakuna tofauti ndani Yake.

271 Alipokutana na Petro, alikutana na Simoni Petro, jina lake lilikuwa Simoni wakati huo, Yeye alimwambia yeye alikuwa ni nani, akamwambia mambo yaliyomhusu. Sasa je, unaamini ya kwamba Mungu anaweza kuniambia kukuhusu wewe, na kukuhusu nafsi yako, na kadhalika namna hiyo? Ingekufanya uamini?

272 Hebu kidogo tu, jambo fulani linatukia. Mama huyo aliyeketi moja kwa moja huko nje, kwenye mkono huo wa kushoto, akiwa na kitovu kilichopasuka, unaamini ya kwamba Mungu atakuponya, Dada? Kama unaamini kwa moyo wako wote, unaweza kupata kile unachoomba.

273 Kuna watu wawili wanaoendelea kusimama hapa. Mtu fulani anamgusa Kuhani Mkuu. Wewe uliyeinua kidole chako

kwenye pua yako hapo, uliyeketi papa hapa, ewe mwanamume, una jongo la moyo, kansa ya ngozi. Yesu alikuponya, Ndugu, imani yako imekuponya.

Aligusa nini? Ni mzee kuliko mtu huyu hapa, ningeweza kuona kulikuwa na tofauti kati yao.

274 Sasa, kama Mungu ataniambia shida yako ni nini, utaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake? Jambo moja, una shida ubavuni mwako, ni namna fulani ya henia, ngiri ubavuni. Hiyo ni kweli. Jambo lingine, una u—ugonjwa wa fadhaa unaokupa shi—shida ya tumbo. Hiyo ni kweli. Sasa, mnaamini, enyi wanaume wote? Huyo alionekana kuwa mtu mzuri.

Hebu na tuchukue muda kidogo na mtu huyu. Tafadhalini mwe na kicho na watulivu.

275 Ana kitu fulani moyoni mwake, unataka Mungu aseme jambo lingine, hiyo ni kweli, maana ninaweza kutambua shauku hiyo. Loo, mbona, ni—ni mwanamke, mke. Amefanyiwa upasuaji, akapata uvimbe kutokana nao. Hiyo ni kweli.

276 Una binti, pia. Huyo binti wakati mmoja aliugua TB, aliponywa kwa uponyaji wa Kiungu. Sasa, ana tumbo lenye fadhaa. Hiyo ni kweli. Wako hapa usiku wa leo, ninawahisi hapo mkutanoni. Watapata afya.

277 Unaamini ya kwamba Mungu anaweza kuniambia wewe ni nani? Ingekusaidia? Kama angaliweza kumwambia Simoni Petro yeye alikuwa ni nani! Umetoka Arkansas, jina lako ni Bw. Blackwell. Nenda nyumbani, Yesu Kristo alikuponya. Shauku zako zimetimizwa, Ndugu.

278 U hali gani, mama? Wewe ni Mwethiopia, mimi ni Muanglo Sakson, hizo ni jamii mbili mbalimbali za watu. Mara ya kwanza kukutana maishani, nadhani. Ikiwa Roho Mtakatifu atanifunulia shida yako ni nini, utaniamini mimi kuwa nanii Wake. . . Ro-. . . Mtakatifu, nabii wa Roho Mtakatifu? Utaamini. Amini tu, usiwe na shaka, amini.

279 Una shauku kubwa moyoni mwako. Unatafuta kwelikweli ubatizo wa Roho Mtakatifu. Hiyo ni kweli. Hilo ni jambo kuu la kutafuta. Kama Mungu anajua jina la mwanamume, Yeye anajua jina la mwanamke, pia. Hivi huamini hivyo? Kama ningekwambia wewe ni nani kwa Roho Mtakatifu, ungeamini basi utampokea Roho Mtakatifu na Mungu atakupa ninii yako. . . Bibi Fitzpatrick, wewe nenda nyumbani, Yesu Kristo atakupa huo ubatizo.

280 Biblia ilisema, katika siku za mwisho, Yesu alisema ya kwamba Ro—Roho angekuja katika siku za mwisho kufanya jambo hili, angekuwa ni Roho yeye yule aliyekuwa juu ya mwili huo wa kibinadamu uliosimama huku mgongo Wake

umeelekezwa kwenye hema katika siku za Ibrahimu. Hiyo ilikuwa ni kweli?

281 Huyu hapa mtu anayefuata amesimama nyuma yangu, ni mwanamke. Je, unaweza kunisikia, mama, wewe uliye nyuma yangu? Vema. Je, anatikisa kichwa chake? Wewe, nitakuangalia. Kama Bwana atanifunulia shida yako, ukiangalia huku, basi unajua ni Malaika yule yule wa Mungu, nguvu zile zile ambazo Yesu alisema zingekuwa hapa katika siku za mwisho. Nyote mtaamini?

Una shida ya kike, shida ya akina mama, shida ya akina mama, shida ya kike. Nenda nyumbani, Yesu Kristo anakuponya. Amini kwa moyo wako wote.

282 Vipi kama nilikwambia Yeye alikuponya, uliyeketi hapo kitini, ukiwa na ugonjwa huo wa moyo, ungeamini? Basi anza tu kuendelea mbele *hivi*, ukisema, "Asante, Bwana." Amini kwa moyo wako wote.

283 Sasa, uko tayari kwa ajili ya upasuaji wa uvimbe huo, lakini je, unaamini ya kwamba Mungu atakuponya? Vema, endelea tu na useme, "Asante, Bwana Yesu."

284 Sasa, hivi hungetaka kwenda kula chakula chako cha jioni usiku wa leo, maskini shida hiyo ya tumbo imeondoka? Ungetaka? Nenda zako ukale, kama unaamini kwa moyo wako wote.

Je, ungetaka kwenda pamoja nami Kalvari kwa ajili ya kupewa damu, kuondoa kisukari? Nenda ukafanye hivyo.

Huyo mama aliyeketi papo hapo nyuma mwenye kisukari anaweza kufanya jambo lile lile, kama tu ukiamini, Dada. Nenda, amini kwa moyo wako wote.

Niliposema ugonjwa wa tumbo muda mfupi uliopita, huo ulikuwa ni wako, pia, kwa hiyo wewe nenda zako tu, ukale chakula chako cha jioni, upate afya.

285 Vema. Mwanamke mkubwa mno, mwenye nguvu namna hiyo, hata hivyo anasumbuliwa na mishipa, hicho ndicho kitu kigumu sana ulimwenguni. Uko huru sasa, Yesu Kristo anakuponya. Nenda, amini kwa moyo wako wote.

286 Maskini msichana, unaamini ugonjwa huo wa pumu utaondoka, nawe utakuwa mzima, na uende nyumbani, upate afya? Endelea tu kutembea, ukisema, "Asante, Bwana."

Ni wangapi wanaoamini kwa moyo wenu wote? Kila mmoja wenu, mwamini Yeye kwa moyo wako wote.

Na wewe je? Unaamini kwa moyo wako wote, unaninii . . .? Endelea tu kutembea. Endelea tu kumsifu Mungu. Mwamini Yeye kwa moyo wako wote.

287 Na wewe je? Unaamini kwa moyo wako wote, Kristo atakuponya? Endelea tu kutembea, ukisema, “Asante, Bwana,” ukiamini kwa moyo wako wote.

288 Unaamini ya kwamba uko sawa, pia? Hutakufa kwa mshtuko wowote wa moyo, endelea tu, amini. Kama ukiamini tu kwa moyo wako wote, utakuwa sawa. Mungu akubariki. Ulitaka nikwambie hilo, kwa hiyo yote yamekwisha sasa, nenda ukiamini kwa moyo wako wote.

289 Ni wangapi wanaoamini kwa moyo wenu wote? Ni wangapi wamechimbua kutokuamini kwote sasa, na kutupa vipande vyote vya kikanisa, nawe uko tayari kumpokea Kristo? Wekeaneni mikono. Hii ndiyo saa ya uamuzi wenu. Tulieni, kila mtu.

[Dada mmoja ananena kwa lugha, ndugu fulani anafasiri—Mh.]

290 Amina. Mnaona yale niliyomalizia kuwaambia? Huduma hii ni mfano wa Eliya aliyetwaliwa juu, naye Elisha alikuwa na sehemu maradufu, sehemu maradufu. Yesu Mwenyewe, aliyemtuma Roho, alisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Mnaona?

291 Nina shaka kama mwanamume huyo na mwanamke huyo wanajuana au la, kuna shaka sana. Huyo mwanamke aliyenena kwa lugha, unamjua mwanamume aliyeifasiri? Kama humjui, inua mkono wako, kama humjui mtu huyo.

Yule aliyefasiri, kama humjui mwanamke huyo, inua mkono wako, huko nyuma kabisa.

292 La, bwana, hakuna mmoja wao anayemfahamu mwingine, nao hawa hapa, walizungumza moja kwa moja pamoja na ujumbe, na kuuleta moja kwa moja hapa kwa ajili ya thibitisho. Ambapo Yesu yupo hapa, anajua siri za moyo, ananena katika karama nyingine namna hiyo, karama ya mahali hapo kupitia karama ya kinabii, kupitia karama ya mahali hapo, kupitia Neno Lake, Huyu hapa. Mbona, jamani, loo, jamani! Utukufu!

293 Wekeaneni mikono, hivyo tu ndivyo mnavyowpaswa kufanya. Gusa kama umetiwa mafuta, na Roho Mtakatifu atakupa.

294 Ee Mungu, katika Jina la Yesu Kristo, lowesha jengo hili kwa Roho Wako. Tupa kila kipande nje, tupilia mbali kila gogo la kale na Mungu wa Mbinguni ajaze na Roho Mtakatifu na kuliwasha moto kanisa hili. Ingia katika Roho wa mkutano huu na kila mmoja wenu aponywe, katika Jina la Yesu Kristo.

295 Haleluya! Mnaamini hilo? Je, uko katika Roho wa kuipokea? Hii ndiyo. Ondolea mbali kila kitu. Kama unaamini kwa moyo wako wote, simama kwa miguu yako na ulikubali, katika Jina la Yesu. Haya basi. Inueni mikono yenu. Utukufu! Utukufu! Amina. Mungu asifiwe!

61-0428 Kuingia Katika Roho
Stephen Mather High School
Chicago, Illinois Marekani

SWAHILI

©2024 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org